SportPesa
CHEZA USHINDE SASA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



**Aliyedaiwa** kuchoma nyumba ya jirani yake auawa, achomwa moto

UKURASA 2



**Fahyma** kweli mapenzi yana wenyewe

UKURASA 20

Nipashe JUMAPILI
MWANGA WA JAMII
Jumapili Oktoba 3, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya
ISSN 0856 • No. 0580722
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Samia amulika maadili vijana

UKURASA 2

## YALIYOMO

UKURASA WA 2
**WASHIKILIWA POLISI TUHUMA KUFANYA MAZOEZI NA FULANA ZA CHADEMA**
JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam linawashikilia wanawake...

UKURASA WA 3
**TAKUKURU YAOKOA MILIONI 48/- ZA MIRADI**
TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Dodoma imesema imeokoa fedha na...

UKURASA WA 7
**ELIMU YA UZALENDO NI MUHIMU KUELEKEA MIAKA 60 YA UHURU**
TUNAPOELEKEA kwenye maadhimisho ya Miaka 60 ya Uhuru na Jamhuri, Desemba 9, mwaka huu, Watanzania...



Mlezi wa Chama cha Skauti Tanzania, Rais Samia Suluhu Hassan, akipokea mwongozo wa kuwawezesha na kuwafundisha vijana wa Skauti jinsi ya kuzuia na kupambana na rushwa, kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (TAKUKURU), CP Salum Hamduni, katika maadhimisho ya Siku ya Mlezi wa Skauti Tanzania, Ikulu ya Chamwino, mkoani Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

## Mwendokasi dereva basi ulivyoua 9, kujeruhi 40

UKURASA 3

RIPOTI MAALUM

## Magulio yalivyo kichaka cha kusambaa kwa corona

UKURASA 4

MICHEZO GOMES: LIGI SASA IMEKUWA VITA UK.24
MAONI, KATUNI UK.6

## Washikiliwa polisi tuhuma kufanya mazoezi wakivaa fulana za CHADEMA

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam linawashikilia wanawake watatu wanaodaiwa kuwa ni wanachama wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) wanaodaiwa walikuwa mazoezini wakiwa wamevaa fulana za chama hicho zenye ujumbe ambao jeshi hilo limelazimika kuwahoji.

Kamanda wa Kanda hiyo, Jumanne Muliro, aliiambia Nipashe jana kuwa wanawashikilia watu hao ambao walikamatwa eneo la Kawe, akiwamo mpigapicha wao kwa maelezo kuwa fulana zao zimebeba ujumbe unaosomeka 'Tunataka Katiba, tunataka tume huru'.

"Kama umefuatilia kwa karibu kila wiki kuna mambo wanafanya, Kibamba walifanya nini na Kinondoni walifanya nini? Wanachokifanya wanawatumia wanawake wanavaa fulana na kujifanya wanafanya mazoezi na ukisikiliza nyimbo zao unaweza kujua ni kitu gani kinachoendelea," alisema.

Kamanda Muliro alisema watu hao wamekuwa wakitumia siku ya Jumamosi ambayo hutumiwa na wananchi kufanya mazoezi kwa kuvaa nguo za chama au fulana zenye maandishi hayo na kuimba nyimbo zinazooana na ujumbe ulioandikwa.

"Kumbuka katika jamii kuna makundi mawili, wanaotaka na ambao hawataki, kwa sababu kila mtu ana chama chake, makundi ya mazoezi ya kawaida watu wanaofanya mazoezi hawashangai, wanawashangaa hawa ambao wapo katika utofauti huo.

"Kwenye mazingira kama hayo, lazima tuingilie kati kuna nini, tunafanya mazoezi, sasa mazoezi gani yenye mitizamo hii? Mbona watu wanawashangaa? Jukumu letu ni kuhakikisha hakuna ugomvi unatokea miongoni mwa watu, kazi yetu ni kuzuia makosa siyo kusubiri kosa litendeke," alisema.

Muliro alisema wanawashikilia watu hao kwa mahojiano ili kujua nia yao ni ipi na wakibaini hakuna makosa, watawaachia.

Kiongozi huyo wa jeshi la polisi alidai kuwa katika tukio hilo wengine walikimbia baada ya kuhisi kuna kitu ambacho ni kinyume.

"Wangekuwa hawana makosa wangesimama, wote walikimbia mbio na walipofika mbele wakazivua fulana zao za chama wakabaki na nguo walizovaa ndani na lengo lao ni kukusanyika eneo la Tanganyika Packers," alidai.

# Samia amulika vijana kupotoka kimaadili

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema licha ya uwapo kwa mifumo ya kuwajenga vijana kimaadili, bado kuna idadi kubwa ya wanaopotoka nchini.

Alitoa kauli hiyo jana katika hafla ya Siku ya Mlezi wa Chama cha Skauti Tanzania iliyofanyika Ikulu Chamwino mkoani Dodoma.

Rais alikitaka Chama cha Skauti, Girl Guides na Umoja wa Vijana wa vyama mbalimbali vya siasa kujiuliza wanapokwama kutokana na kuwa na idadi kubwa ya vijana ambao wana ukosefu wa maadili.

"Ukiangalia mfumo wa Skauti, wa Umoja wa Vijana wa Chama cha Mapinduzi (UVCCM), umoja wa vijana wa vyama vingine vya siasa, Girl Guides wetu, ukosefu wa maadili unatoka wapi Tanzania ikiwa tuna taasisi zote hizi zenye mifumo mikubwa ya kulea vijana lakini bado tuna idadi kubwa ya vijana wanaopotoka?

"Tujiulize tumekwama wapi, tumekosea wapi na hilo swali naliacha kwa taasisi zote nilizozitaja hapa, tujiulize tunakwama wapi, kwa nini vijana wetu wapotoke wakati tuna mifumo yote hii?" Rais alihoji.

Alisema mfumo wa Skauti ni mkubwa na unaendana na serikali na kuahidi kuimarisha zaidi chama hicho ambacho kinawaunganisha vijana bila kujali dini, kabila, rangi au itikadi ya vyama vya siasa.

Rais Samia alibainisha kuwa chama hicho ni muhimu kuwalea vijana kwenye maadili mema, ukakamavu na kuwaandaa viongozi wajao wa taifa.

"Umuhimu huu wa Skauti umeongezeka zaidi katika kipindi hiki cha utandawazi na maendeleo ya sayansi na teknolojia, endapo hatutawaandaa vijana wetu, upo uwezekano mkubwa wa kurubuniwa na kuangukia kwenye vitendo au makundi maovu," alitahadharisha.

Rais Samia aliongeza: "Baraza la Skauti liendelee kuwafundisha kiapo na kanuni hizi watoto wetu wanapojiunga, mjitahidi kuwachukua wakiwa na umri mdogo, tukiweza kuwafundisha kwa watoto wadogo jambo hili litakaa, Skauti wengi wakiingia kwenye ajira zao huwezi kuta wanahujumu, kuiba au kufanya kinyume cha maadili."

Aliwataka Skauti wa Tanzania kuishi kwa kiapo na vitendo na kuwa mfano kwa jamii ili kuhamasisha wengine kujiunga.

Hata hivyo, Rais Samia aliwataka kubeba ujumbe wa kuhamasisha na kuelimisha watu kubadili mawazo yao na kuwa na hiari ya kuchanjwa ili kujikinga na vifo na ukali wa maradhi ya corona.

"Lingine, mwakani nchi yetu itaingia kwenye kuhesabu watu, watanzania tujuane tupo wangapi kwenye maeneo yapi, zoezi litaingia makazi ya Watanzania, tuna majumba mangapi ya aina gani, yapo wapi? Tutaweka mipaka kwenye vitongoji na vijiji na kujiepusha na migogoro inayokuja wakati wa uchaguzi wetu.

"Pia sensa inaenda kutusaidia kuweka anuani baada ya kujua makazi, tunaomba Skauti msaidie na ikibidi mjitoe kwenda kusaidia zoezi hili liende vizuri," alisema.

Kuhusu uhaba wa fedha za kuendesha shughuli za Skauti, Rais Samia alikipongeza chama hicho kwa kubuni na kutafuta suluhisho la kero kwa kuweka vitega uchumi ambavyo vitatumika kuinua uchumi wao na kuahidi kuwaunga mkono.

"Kuhusu kuirudisha Skauti kwenye bajeti ya Wizara ya Elimu, jambo ambalo sitaki kuahidi hapa tutalifanyia kazi, tukiingiza kwenye wizara, Girl Guides watakuja waingizwe, vyama vingine watakuja waingizwe, nitakachofanya ni kuangalia mbinu za kusaidia kufanya kazi yenu lakini sio kuwarudisha.

"Nafasi za uteuzi mfano mzuri RAS (Katibu Tawala wa Mkoa) wa Kigoma yupo hapa, bila shaka kuna Skauti wengi wameteuliwa lakini hawajavaa sare lakini tumechukua tutazingatia, ila wanapojaza CV (wasifu) hawasemi kama ni Skauti, wanaandika sifa za shule, unajikuta unateua Skauti hujui kama ni Skauti," alisema.

Awali, Skauti Mkuu wa Tanzania, Mwamtumu Mahiza, alisema zaidi ya Sh. bilioni 34 zinahitajika kulipa fidia, kujenga majengo na vifaa vya kujifunzia kwenye jengo litakalojengwa Dodoma.

"Ninakuomba Rais ambaye ndiye Mlezi wa Skauti kuwezesha kupata fedha hizo ili mradi huo uanze na chama kijitegemee," alisema.

Awali, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Simai Mohammed Said, alisema Serikali ya Zanzibar ipo kwenye mchakato wa kuwapatia eneo la Kijiji cha Skauti.



Katibu Mkuu wa Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA), Nuhu Mruma (kushoto) na Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu Huria cha Kimataifa nchini Gambia, Dk. Cherno Barny, wakibadilishana nyaraka baada ya kutiliana saini makukabiliano ya utoaji elimu ya chuo kikuu kwa njia ya mtandao, jijini Dar es Salaam jana. Katikati ni Mufti wa Tanzania Sheikh Abubakar Zuber. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Adaiwa kuchoma nyumba ya jirani, naye achomwa

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

MKAZI wa Kijiji cha Dakawa, Kata ya Bwakila Chini, Juma Katinda (58), ameuawa na kundi la watu wenye hasira kali ikidaiwa ni kulipiza kisasi baada ya kutuhumiwa kuchoma moto nyumba ya jirani yake.

Kutokana na tukio hilo la mauaji, watu 20 wanashikiliwa na Jeshi la Polisi kwa ajili ya uchunguzi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Fortunatus Musilim, alisema jana kuwa mauaji hayo yalitokea Septemba 29, mwaka huu saa 11 jioni katika maeneo ya Kitongoji cha Mgamba, Kijiji cha Dakawa katika Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro.

Alibainisha kuwa kutoka na tukio hilo, msako wa jeshi hilo ulifanywa na kufanikisha kutiwa mbaroni kwa watu 20 wakituhumiwa kuhusika na mauaji hayo kwa kujichukulia sheria mkononi, wakiwamo wanane waliokamatwa ndani ya basi katika harakati za kutoroka kijijini huko. Kamanda Musilim alisema watuhumiwa hao wanadaiwa kumshambulia Katinda kwa kumpiga na kumsababishia kifo na baadaye kuuteketeza mwili wake kwa moto umbali wa mita 200 kutoka eneo ambalo alidaiwa kuchoma nyumba.

Awali, ilidaiwa kuwa Katinda alichoma moto nyumba ya jirani yake aliyetajwa kwa jina moja la Ruchamla kwa madai kuwa eneo ilikojengwa nyumba hiyo ni lake na ilijengwa wakati akiwa safarini kwa muda mrefu.

"Awali wananchi walijitokeza kwenda kutoa msaada wa kuzima moto nyumba iliyochomwa lakini Katinda aliwazuia wasitoe msaada ndipo wananchi wakaitana kwa wingi na kumzingira kisha kumshambulia kwa silaha za jadi na kumuua na mwili kuuteketeza kwa moto," alidai Kamanda Musilim.

Kiongozi huyo wa Jeshi la Polisi aliitembelea familia ya mwenye nyumba iliyochomwa moto na kuwapa pole pamoja na familia ya marehemu iliyookolewa wakiwamo wake zake watatu, watoto, ndugu na jamaa wanaofikia 11 waliopelekwa kuhifadhiwa Kituo cha Polisi Duthumi kwa ajili ya usalama wao.

Katika mkutano na wananchi wa Kata ya Bwakila Chini ambao ulihudhuliwa na viongozi mbalimbali wa kijiji hicho, Kamanda Musilim aliwataka wananchi kuachana na vitendo vya kujichukulia sheria mikononi badala yake watoe taarifa kwenye vyombo vya dola kuhusu matukio yoyote ya kiuhalifu.

# ‘Usalama barabarani uwe ajenda mtambuka’

**Na Mary Geofrey**

MTANDAO wa Asasi za Kiraia unaoshawishi maboresho ya Sheria ya Usalama Barabarani, umeishauri serikali na wananchi kuliangalia suala la usalama barabarani kuwa ajenda mtambuka na shirikishi inayomgusa kila mmoja na siyo suala la Jeshi la Polisi na taasisi zake.

Rai hiyo ilitolewa juzi jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi Mkuu wa Chama cha Wanasheria Wanawake (TAWLA), Tike Mwambipile, katika mkutano na wadau wake kwa lengo la kujadili maboresho ya Sheria ya Usalama Barabarani ya Mwaka 1973.

Alisema pia wanaishauri serikali kuendelea kushirikiana na wadau katika matukio na maadhimisho mbalimbali ya kikanda na kimataifa kwa ajili ya kuendelea kuongeza uelewa wa ajali na madhara kwa wananchi.

“Tunatoa wito kwa serikali na wadau wengine wa maendeleo nchini kuiwezesha sekta hii ya usalama barabarani na siyo kutegemea wafadhili wa nje,” alisema.

Tike alisema mtandao huo unashawishi maboresho ya Sheria ya Usalama barabarani kuhusu mwendokasi, matumizi ya vizuizi vya watoto, kofia ngumu, mikanda, vilevi na matumizi ya vifaa vya kieletroniki.

Alisema katika kipindi cha miaka sita tangu kuanzishwa kwa mtandao huo, wamefanikiwa kuendesha kampeni ya ushawishi kutetea maboresho ya sheria hiyo.

Tike alisema pia wameongeza ufahamu kwa umma kuhusu masuala ya usalama barabarani.

“Wanamtandao tunaamini kwamba suala la usalama barabarani licha ya kutopewa uzito mkubwa katika jamii zetu, bado ni eneo linalogharimu maisha ya watu, linasababisha ulemavu na hata kudidimiza uchumi.

“Kwa mfano, kulingana na takwimu za Shirika la Afya Duniani (WHO), watu milioni 1.35 hufariki dunia kila mwaka kutokana na ajali hizo,” alibainisha.

Mkurugenzi huyo pia alisema katika kipindi hicho wameimarisha na kuboresha uhusiano na serikali kupitia Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, Wizara ya Katiba na Sheria na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii Jinsia, Wazee na Watoto.




Watoto wa mtaani wakiosha kioo cha gari ili kujipatia riziki kwenye foleni ya magari katika Barabara ya Bagamoyo, eneo la ITV, Manispaa ya Kinondoni, mkoani Dar es Salaam jana. Malipo ya kazi hiyo, hutegemea huruma ya mwenye gari. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Mwendokasi dereva wa basi ulivyoua tisa na kujeruhi 40

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WATU tisa wamefariki dunia na wengine 40 kujeruhiwa kwenye ajali ya basi la abiria la Kampuni ya Emigrace lenye namba za usajili T 703 DLG lililokuwa likitokea Babati mkoani Manyara kwenda Dar es Saalam, kupinduka huku chanzo kikitajwa kuwa ni mwendokasi na kufeli kwa breki.

Kwa mujibu wa taarifa za awali zilizotolewa na Jeshi la Polisi Mkoa wa Dodoma zinadai kuwa basi hilo lilifeli breki na kupinduka katika eneo la Mlima Kolo wilayani Kondoa mkoani hapa jana majira ya saa 1:20 asubuhi.

Dereva wa basi hilo ambaye jina lake halikupatikana, alidaiwa kukimbia mara tu baada ya ajali hiyo kutokea.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Best Magoma, akizungumza na waandishi wa habari kwa njia ya simu kutoka eneo la tukio, alithibitisha kutokea kwa ajali hiyo iliyosababisha vifo vya watu tisa na majeruhi 40. Alisema kuwa katika ajali hiyo, watu wanane walipoteza maisha katika eneo la tukio na mmoja alifariki dunia wakati akipatiwa matibabu katika Hospitali ya Wilaya ya Kondoa.

“Mpaka hivi sasa (jana saa tisa alasiri) vifo ni watu tisa ambapo wanane walifariki duniani palepale na mmoja aliongezeka wakati akipata matibabu lakini pia tumepokea majeruhi 40 ambapo 22 wametibiwa na kuruhusiwa, wengine 15 tumewapatia rufani ya kwenda Hospitali ya Mkoa wa Dodoma kwa matibabu zaidi,” alifafanua Dk. Magoma.

Mmoja wa majeruhi aliyepewa rufani kwenda Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma, Asiatu Mbwambo, alidai kuwa kabla ya kupata ajali hiyo, dereva alikuwa akiendesha kwa mwendokasi.

“Alikuwa anakwenda kasi sana kwenye kona za Mlima wa Kolo hadi tukampigia kelele, alifikia hatua akakasirika, akasimamisha gari na kusema tusimfundishe kazi.

“Baada ya muda mfupi, niliyekuwa nimekaa naye jirani akaniambia tunaanguka, toka hapo sikujua kilichoendelea hadi mpaka ninajikuta hospitalini,” alisema.

Mkazi wa Kikiji cha Bukuru wilayani Kondoa, Yahaya Oliye, alisema ndugu zake sita walipanda basi hilo kwenda mkoani Dar es Salaam na kati yao, mmoja amepoteza maisha katika ajali hiyo.

“Ndugu zangu hawa walikuja kusalimia nyumbani, leo (jana) walikuwa wanaondoka, niliwasindikiza na kupanda basi hili lakini baada ya muda mfupi mmoja alinipigia simu na kusema kuwa gari limepinduka, wanaomba msaada ndio tukatoka na pikipiki kwenda kuwaona,” alisema. Mkurugenzi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma, Dk, Ernest Ibenzi, alisema wamepokea majeruhi 10 ambao wengi wao wameumia katika maeneo mbalimbali ya miili yao.

“Wameletwa majeruhi 10 mpaka sasa hapa kwetu na wengine tayari tumeshawapeleka katika chumba cha upasuaji. Kati yao, wanawake ni sita na wanaume wanne,” alibainisha Dk. Ibenzi.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya CHAMWINO.**

**Kituo cha HANETI Mkoa DODOMA.**

**Usimamizi wa mirathi Na 01 /2021.**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU EMANUEL MAYUNGA WA CHENENE**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA AGUSTINO MAYUNGA**

**TANGAZO**

(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)
Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na Mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 22 mwezi 10 mwaka 2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
**Imetolewa leo tarehe 01 mwezi 10 mwaka 2021.**

HAKIMU

HAKIMU MAHAKAMA YA MWANZO HANETI DODOMA

116489102


# TAKUKURU yaokoa milioni 48/- za miradi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Dodoma imesema imeokoa fedha na vifaa vyenye thamani ya jumla ya Sh. milioni 47.8, vikiwamo vya Sh. milioni 41,8 vilivyochepushwa kutoka kwenye mradi wa ujenzi wa hospitali.

Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Dodoma, Sosthenes Kibwengo, alisema juzi jijini hapa kuwa hatua hiyo imetokana na ukaguzi wa miradi 17 ya sekta za elimu, afya na kilimo uliolenga kuhakikisha fedha za umma zinazoelekezwa kwenye miradi mbalimbali, zinatumika kwa ufanisi na uaminifu.

Alisema katika kuhakikisha thamani halisi ya fedha inapatikana, taasisi hiyo kwa kushirikiana na Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) na Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) inaendelea kuelekeza nguvu katika kufuatilia utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa barabara na maji kwa kuzuia vitendo vya rushwa na kufanya utambuzi wa mianya ya rushwa unaolenga kutoa ushauri wa namna ya kuziba mianya hiyo.

Kibwengo alibainisha kuwa Agosti mwaka huu, TARURA Mkoa wa Dodoma ilitia saini mikataba 43 na makandarasi mbalimbali kwa kazi ya ujenzi wa barabara katika wilaya zote za Mkoa wa Dodoma zenye thamani ya jumla ya Sh. bilioni 10.2 ikiwa ni miradi ya awamu ya kwanza itakayotekelezwa kwa mwaka 2021/22.

“RUWASA iligawanya mabomba yenye urefu wa mita 35,232 katika wilaya zote za Dodoma kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa mpango wa malipo kwa matokeo awamu ya nne ambapo gharama za ulazaji wa mabomba hayo zinakadiriwa kuwa zaidi ya Sh. milioni 95,” alisema.

Sambamba na hayo, alisema katika kipindi cha robo iliyoisha, jumla ya taarifa 120 zimepokewa na taasisi hiyo ambapo taarifa za rushwa zilikuwa 76 huku taarifa sita kati ya hizo zikihamishiwa idara nyingine.

“Uchunguzi wa majalada 10 ulikamilika na mashauri tisa yakafunguliwa mahakamani ambapo mashauri sita yalitolewa hukumu na Jamhuri imeshinda mashauri matatu na kushindwa matatu,” alifafanua.

Kibwengo alisema kuwa katika robo mwaka inayofuata, yaani Oktoba hadi Desemba mwaka huu, TAKUKURU itatumia mbinu ya kuwashirikishwa vijana katika mapambano dhidi ya rushwa kupitia ushirika wa UTATU WA TAKUKURU.

Alikumbusha kuwa utatu huo unajumuisha Chama cha Skauti Tanzania pamoja na Idara ya Elimu kwa kuwaelimisha kuhusu mbinu na umuhimu wa kushiriki katika kuzuia rushwa ili nao wafikishe elimu nyumbani na jamii kwa ujumla wake.

“Kazi yetu ni kuhakikisha jamii inakuwa salama dhidi ya vitendo vya rushwa, tunaendeleza mapambano kupitia programu yetu ya TAKUKURU INAYOTEMBEA kwa kufuata wananchi na kusikiliza kero zao zinazohusiana na rushwa na kuzitafutia ufumbuzi. Vilevile, tutaendelea na jukumu la kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika mkoa wetu,” alisema.


bgtl **BEST GROUP (T) LIMITED**
Debts collectors, Auctioneer, Commission Agent & Legal Consultant

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

*Kwa Idhini tuliyopewa* na ***BANK OF AFRICA*** Tunatoa notisi ya siku kumi na nne(14) kuanzia Tarehe ya Tangazo hili kwa mdaiwa aliyetajwa hapo chini, alipe deni analodaiwa na benki hiyo pamoja na riba. Kushindwa kulipa kwa muda huo tutalazimika kuuza dhamana (mali) iliyodhaminiwa mkopo wake kwa **MNADA WA HADHARA.** Mnada utafanyika kuanzia saa 4:00 Asubuhi na kuendelea mahali dhamana ilipo kama inavyoonesha hapo chini.

| Na. | JINA LA MDAIWA | JINA LA MDHAMINI | DHAMANA NA MAHALI ILIPO |
|---|---|---|---|
| 1 | ALISON MBONYO | ALISON HASHIM MBONYO | Nyumba ya makazi yenye Hati ya usajili na.16646LR Kiwanja na.107 kitalu”A” iliyopo Mapinduzi mkoa wa Dodoma |

**MASHART YA MNADA**
1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa siku ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14). Kukamilisha malipo yote. Kushindwa kufanya hivyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25%, na mnada kurudiwa, au mshindi wa pili atapewa ushindi.
4. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/mpangaji na zingine zinazoambatana na hilo ni jukumu la mnunuzi.

**Kwa Taarifa zaidi wasiliana na:**
**Mkurugenzi Mtendaji**
**Best Group (T) Ltd**
**Alli Hassan Mwinyi Road**
**Green Acres Buliding, 2nd Floor**
**P.O. BOX 1088**
**Dar Es Salaam.**
**Mob: + 255 715-363537/ +255 765-363537**

**AU**

**Mkurugenzi Mtendaji**
**Bank of Africa**
**Head Office,**
**NDC Development House, Ohio street/kivukoni**
**P.O. BOX 3054,**
**Dar Es Salaam, Tanzania.**
**Tel: +255-22-2110104/2111290**
**Fax: +255-22-2113740**

116489902

RIPOTI MAALUM

# Magulio yalivyo kichaka cha kusambaa kwa corona

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

ELFU mbili pale, naongeza elfu moja, elfu tatu pale! Elfu tatu kwa mara ya kwanza, mara ya pili elfu tatu, elfu tatu kwa mara ya mwisho, haya daka hiyo!" Ni maneno yanayosikika kutoka kwa mmoja wa wafanyabiashara wanaorusha nguo kwa wateja wao kwenye gulio la mitumba lililoko katika Soko la Sabasaba jijini Dodoma.

Soko hili ni maarufu kwa uuzaji wa bidhaa mbalimbali ikiwamo vitu na nguo za mitumba na ndani yake kuna gulio la nguo ambalo hufanyika kila siku nyakati za asubuhi.

Udadisi wa Nipashe Jumapili umebaini wafanyabiashara wadogo, maarufu machinga, ni miongoni mwa wateja wakubwa wa gulio hilo la 'kurusha na kudaka nguo' kulingana na bei ambayo mteja anaitaja na kumridhisha mrushaji.

Hata hivyo, wakati serikali ikiendelea na mikakati mbalimbali kukabiliana na mlipuko wa virusi vya corona vinavyosababisha ugonjwa wa UVIKO-19, uchunguzi wa Nipashe Jumapili uliofadhiliwa na taasisi ya habari ya Chimbua Communication, umebaini mkusanyiko mkubwa wa watu kwenye gulio hilo unakwenda kinyume cha miongozo iliyotolewa na serikali ili kudhibiti kuenea kwa virusi hivyo.

Miongozo mbalimbali iliyotolewa na serikali kukabiliana na maambukizo mapya ya corona, inajumuisha kuzuia mikusanyiko mbalimbali na kuhimiza kuzingatia masharti ya uvaaji barakoa na kunawa mikono, lakini hali ni tofauti katika gulio hilo.

Nipashe Jumapili imebaini kuwa licha ya wataalamu wa afya kuhimiza juu ya kuchukua tahadhari dhidi ya wimbi la tatu la corona, maarufu Delta, wafanyabiashara hao wanafanya biashara zao bila kuzingatia tahadhari hizo.

Ripoti ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ya mwezi uliopita, ilibainisha kuwa hadi Septemba 30, mwaka huu, kulikuwa na vifo vya watu 719 nchini kutokana na UVIKO-19 huku maambukizi ya virusi hivyo yakifikia watu 25,846. Pia watu 45 walikuwa wakipumua kwa msaada wa mashine.

Toleo la kwanza la mwongozo wa udhibiti wa UVIKO-19 kupitia afua ya kudhibiti misongamano katika jamii bila kuathiri shughuli za kiuchumi la Julai, 2021 lililotolewa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Prof. Abel Makubi, linaainisha mambo yanayohitajika kuzingatiwa kwenye masoko, magulio, minada, maduka makubwa na maeneo mengine ya biashara.

Mambo hayo ni pamoja na halmashauri ziandae timu za kukagua maeneo hayo na timu hizo zijumuishe viongozi wa ngazi za jamii



**719**

Idadi ya watu waliofariki dunia kutokana na UVIKO-19 nchini.

ili kupunguza misongamano katika maeneo husika.

Mwongozo huo pia unazitaka halmashauri ziainishe maeneo zaidi na kuangalia namna ya kupunguza msongamano ikiwa ni pamoja na kutumia viwanja vya mipira wa miguu au maeneo yoyote yaliyo wazi kwa ajili ya huduma za masoko au kushushia bidhaa, ili wafanyabiashara na wateja wawe katika umbali unaokubalika na kuweka utaratibu kwa wateja kukaa umbali wa mita moja au zaidi wakati wa kupata huduma.

Vilevile, mwongozo unataka kuwekwa utaratibu kwenye maeneo ya kuingilia ili kuhakikisha kila mteja na mfanyabiashara anayeingia kupata huduma katika maeneo hayo awe amevaa barakoa au aelekezwe kununua barakoa bila shuruti.

Mwongozo huo pia unamtaka kila mwenye biashara aweke chombo chenye maji tiririka na sabuni na kila mara awaelekeze wateja wake kunawa kabla hawajaingia sokoni au dukani kupata huduma na watu wasiokuwa na kazi maalum wasiruhusiwe kukaa katika maeneo hayo ili kupugunguza msongamano na minada iepuke shughuli zinazofanya watu kukaa muda mrefu na kuchangamana zaidi.

**HALI ILIVYO**

Licha ya kuwapo kwa mwongozo huo, Nipashe Jumapili imebaini kuwa katika gulio hilo la Sabasaba wafanyabiashara hao hawavai barakoa, hawanawi mikono wala kujiepusha na msongamano.

Katika mazungumzo na gazeti hili, Josephine Kuyanga, mmoja wa wafanyabiashara anasema kutokana na eneo lilivyo na watu kubanana wakigombea kudaka nguo, ni vigumu kuzingatia masharti hayo.

"Unajua hili eneo ni kama kugombea nguo fulani ambayo umevutiwa nayo, na kwa jinsi eneo lilivyo, ukivaa barakoa ni kujikosesha pumzi. Kwa kweli ni ngumu kuzingatia masharti hayo wanayosema wataalamu," anasema.

Selemani Hassan, mteja wa bidhaa hizo aliyekutwa na mwandishi kwenye gulio hilo, anasema awali uliwekwa utaratibu wa kulazimisha kuingia kwenye gulio wakiwa wamevaa barakoa na kunawa mikono, lakini wakiingia ndani hali ni tofauti kulingana na mazingira ya gulio hilo. "Unaingia umevaa barakoa, unakutana na msongamano wa watu wengi, hata hewa tu hakuna ya kutosha, ukitaka nguo unanyoosha mkono unaletewa. Je, yule anayepokea hela mikono yake amechukua tahadhari? Kwa kweli kwenye hili soko ni vigumu sana kuzingatia hiyo miongozo ya kukabili corona," analalamika.

Hassan ana ushauri kwa mamlaka husika kwamba kwa sasa ni vyema gulio hilo likafanyika kwenye eneo la nje ya soko ili kuwa na hewa ya kutosha na kupunguza msongamano wa watu.

**UONGOZI WA SOKO**

Mwenyekiti wa Soko la Sabasaba, Athumani Makole, anasema tayari walishaweka taratibu kwenye soko hilo kwamba hakuna mtu yeyote atakayeingia sokoni pasi na kuvaa barakoa ili wananchi wajikinge na maambukizi ya virusi vya corona.

Anasema wameandaa mkakati huo kwa kushirikiana na Ofisa Afya wa Kata ya Viwandani na wametangaza kuwapo kwa mgambo kwenye lango la kuingia sokoni.

"Tumeweka maji tiririka kila mlango wa kuingilia, tumeweka vitakasa mikono na kila mlango kuna watu ambao wanauza barakoa na zaidi ya yote kuna mgambo kila mlango ambaye kazi yake kubwa ni kuwazuia watu wasiokuwa na barakoa wasiingie ndani ya soko.

"Hatuwezi kuwa wapole kwa jambo hili, ni bora tuwe wakali watu watuchukie kuliko kuwa wapole na kutafuta sifa wakati watu wanaangamia," anasema Kombo.

**25,846**

Idadi ya watu walioambukizwa virusi vya corona nchini.

Ofisa Afya wa Kata ya Viwandani jijini humo, Fausta Kibiti, anasema wanaendesha operesheni ya kuwadhibiti wasio vaa barakoa na kuzingatia maelekezo ya wataalamu wa afya kuhusu kujikinga na ugonjwa huo kwenye soko hilo.

"Tumekuwa na operesheni kwa wale ambao wanauza mitumba kwa kuwataka wavae barakoa na wanaokaidi wanatolewa na mgambo ndani ya soko, tunatoa elimu juu ya umuhimu wa kuvaa barakoa na ikumbukwe kuwa katika magulio kuna msogamano mkubwa ambao ni hatari kwa afya ya watoa huduma na wapokea huduma. "Hili zoezi ni endelevu na ni lazima lifanyike mara kwa mara kwa faida ya wafanyabiashara na wanaopata mahitaji kwenye Soko la Sabasaba," anasema.

**MIKAKATI YA SERIKALI**

Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Prof. Makubi, anasema licha ya kutoa mwongozo wa kujikinga dhidi ya virusi hivyo, serikali inaendelea kutoa elimu kwa wananchi sehemu zote ili kuchukua tahadhari za kujikinga na ugonjwa huo bila kuathiri shughuli za maendeleo.

Anasema mbali na elimu hiyo, serikali pia inahimiza wananchi kupata chanjo ya UVIKO-19.

Julai mwaka huu, Rais Samia Suluhu Hassan alizindua utoaji chanjo kitaifa ambapo dozi zaidi ya milioni moja zilipokewa nchini na hadi kufikia Septemba mwaka huu, serikali ilibainisha kupitia kwa Msemaji Mkuu, Gerson Msigwa, kuwa zaidi ya watu 400,000 walikuwa wamepata chanjo hiyo.

Hata hivyo, kutokana na idadi ndogo ya waliopata chanjo, Wizara ya Afya imekuja na mpango wa jamii shirikishi na harakishi wa chanjo dhidi ya UVIKO-19 wenye mambo 10, ikiwamo kuwapo kwa chanjo tembezi kwa kuwafuata wananchi walio tayari kuchanjwa kwa hiari. Kwa mujibu wa Prof. Makubi, mpango huo unaokwenda sambamba na kuongeza vituo vya kuchanja kutoka 550 hadi kufikia 6,784, unalenga kuhakikisha wananchi wanachanjwa mapema, ukisimamiwa na wakuu wa mikoa, makatibu tawala wa mikoa na waganga wakuu wa mikoa.

"Tunahitaji wananchi wachanje mapema iwezekanavyo kutokana na asili ya ugonjwa wenyewe. Katika mpango huu elimu itolewe kupitia njia za asili za ngoma, kwaya, muziki, maigizo, semina, mikutano na pia TV na redio jamii, kutumia pia viongozo wa serikali, kijamii, kidini, wabunge, wasanii, watu maarufu, wataalamu na wawakilishi wa vikundi vya kijamii kama vile Vicoba" anafafanua.

Prof. Makubi pia anasema elimu inayoambatana na utoaji chanjo itafanyika kwenye maeneo yote yenye mikusanyiko ikiwamo kwenye magulio na minada.

**MBINU ZA KENYA**

Mwandishi wa habari wa Kenya, Dancan Maiche, katika mazungumzo na Nipashe Jumapili kujua kinachofanyika kwenye taifa hilo jirani kukabili corona, anabainisha kuwa Machi mwaka jana, Serikali ya Kenya ililazimika kupiga marufuku uingizaji wa nguo za mitumba ili kuepusha kuenea kwa virusi vya corona. Anakumbusha kuwa kipindi hicho (Machi mwaka jana) kulikuwa na kasi kubwa ya maambukizi katika nchi za Ulaya ambako Kenya huagiza nguo hizo.

Hata hivyo, Maiche anabainisha kuwa Agosti mwaka jana, serikali yao iliondoa katazo hilo kwa kuweka masharti mbalimbali ya kufuatwa ikiwamo nguo hizo kupuliziwa dawa kabla ya kuuzwa na pia kuelekeza ziuzwe kwa njia ya mtandao ili kuondokana na msongamano wa watu kwenye magulio.

Kwa mujibu wa Takwimu za Shirika la Afya Duniani (WHO), mlipuko wa virusi hivyo bado ni tishio duniani na umegharimu maisha ya watu wengi kutokana na virusi hivyo kujibadili sura. Takwimu za shirika hilo zinaonyesha kuwa hadi mwishoni mwa mwezi uliopita, zaidi ya watu milioni 223 walikuwa wameambukizwa virusi vya corona duniani na zaidi ya milioni 4.6 wamefariki dunia kutokana na ugonwja wa UVIKO-19.

Virusi vya corona vinavyosababisha ugonjwa wa UVIKO-19 viliripotiwa kwa mara ya kwanza Wuhan, China Novemba 2019. Tanzania iliripoti kupata mgonjwa wa kwanza wa virusi hivyo Machi 16 mwaka jana.

HABARI KITAIFA

# Wadau wachangia mil. 30/- ununuzi wa mashine tiba

**Na Mary Geofrey**

DIWANI wa Kawe mkoani Dar es Salaam, Mutta Rwakatare, ameishukuru Rotary Club Tawi la Mbezi Beach kwa kuendesha kampeni ya kuchangisha fedha kwa ajili ya kununua vifaa vya matibabu katika Zahanati ya Kawe.

Club hiyo imelenga kuchangisha Sh. milioni 90 kwa awamu tatu kwa ajili ya kununua vifaa vya matibabu ikiwamo mashine ya Utra Sound na gari la kubebea wagonjwa.

Rwakatare, akizungumza jana muda mfupi baada ya kumalizika kwa michezo mbalimbali ya kuhamasisha uchangiaji huo, alisema kuchangishwa kwa fedha hizo kutasaidia kuokoa maisha ya watu wengi wanaokosa huduma muhimu katika zahanati hiyo.

"Ninaishukuru Rotary Club ambao ni wadau wetu wakubwa wa maendeleo wanaotusaidia katika Sekta ya Afya. Kuwapo kwao leo hapa kutasaidia kukusanya fedha kwa ajili ya kununua mashine ikiwamo ya Ultra Sound ili kusaidia wananchi kupata vipimo katika zahanati hiyo," alisifu.

Rais wa Rotary Club, Pamela Mutabasi, alisema kupitia michezo waliyoshiriki jana, walilenga kukusanya Sh. milioni 30 ili kuchangia vifaa vya matibabu katika zahanati hiyo.

Alisema katika club yao wameweka vipaumbele viwili katika Shule ya Msingi Kawe na Zahanati ya Kawe kwa ajili ya kutatua kero mbalimbali zinazowakabili wananchi.

"Fedha hizi ambazo tunachangisha leo (jana) hapa zitasaidia kununua mashine tatu za kutolea huduma katika Zahanati yetu ya Kawe ikiwamo mashine ya Ultra Sound.

"Awamu ya pili tunatarajia kukusanya tena Sh. milioni 30 na baadaye awamu ya tatu tutamalizia kukusanya tena kiasi hicho cha fedha," alisema.

Alisema Rotary ni mtandao wa kimataifa unaojumuisha majirani, marafiki na viongozi na kwamba wamekuwa wakifanya kazi za kujitolea kwa jamii kwa zaidi ya miaka 110 katika sekta za elimu, afya, maji, kudumisha amani, afya ya mama na mtoto pamoja na kukuza vipato kwa wenye vipato duni.

# Utouh: Vijana washiriki kuandaa bajeti ya serikali

**Na Halfan Chusi**

MKURUGENZI wa Taasisi ya WAJIBU inayojihusisha na masuala ya uwazi na uwajibikaji, Ludovick Utouh, ameshauri vijana washirikishwe katika uaandaji wa bajeti kuanzia ngazi ya chini hadi kitaifa.

Utouh aliyewahi kuwa Mdhibiti ba Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), alitoa rai hiyo mkoani Dar es Salaam juzi alipokutana na wananvyuo ambao wapo ndani ya klabu za uwajibikaji na kufanya majadiliano nao juu ya mambo kadhaa ikiwamo uwajibikaji wao katika upangaji wa bajeti.

Mkurugenzi huyo alisema vijana wengi wamekuwa hawahusishwi katika suala zima la upangaji bajeti kuanzia ngazi ya chini hadi kitaifa.

Alisema vijana wana nafasi kubwa ya kuiletea nchi maendeleo chanya kama watapewa nafasi ya kushiriki katika upangaji wa bajeti katika ngazi zote ikiwamo serikali za mtaa, kata hadi katika ngazi za kitaifa. "Vijana ndio watu wenye ushawishi mkubwa katika jamii. Maendeleo yao yanaendana na mipango ya bajeti itakayopangwa pamoja lakini pia wana nafasi ya kuelimisha Watanzania wengine ili taifa liweze kisonga mbele," alisema.


Utouh aliongeza juwa mwaka ujao utakuwa wa Sensa ya Watu na Makazi, hivyo vijana bado wana nafasi kubwa ya kuhamasisha watu kujitokeza kwa wingi kuhesabiwa ili serikali ijue idadi halisi ya watu waliopo nchini ili kuipa nafasi serikali kupanga bajeti kuendana na idadi ya watu waliopo.

Katika hafla hiyo, pia kulikuwa na ugawaji wa zawadi kwa wananvyuo 23 kutoka vyuo mbalimbali walioshiriki katika kuandika insha nzuri iliyohusu njia za kusaidia kuongeza ushiriki wa vijana kwenye uandaaji wa bajeti ya taifa.

Kati ya hao 23 walioshiriki, Raymond Manyenye kutoka Chuo Kikuu cha Mipango Dodoma, aliibuka mshindi katika kinyanganyiro hicho akifuatiwa na wengine wa nne katika nafasi ya tano bora huku wengine ambao hawakufanikiwa kushinda, wakipongezwa kwa kushiriki kwa kupewa zawadi ya cheti na kitabu kilichondikwa na Ludovickh Utouh, kinachozungumzia zaidi uwajibikaji kwa vijana. Mkurugenzi Mtendaji wa Msichana Initiative, alisema zaidi asilimia ya watu nchini ni vijana, hivyo kuna kila sababu ya kuwatumia vijana katika kutoa uamuzi.

"Ninashukuru sana kualikwa na WAJIBU, kwangu hii ni heshima kubwa sana, ni jambo muhimu sana hasa tunapoangalia vijana kushiriki, kwa hiyo ni muhimu kama hivi kuwakutanisha vijana na kuwapa elimu.

"Nitoe rai kwa jamiii kupitia vyombo vya habari pale vijana tunapopata nafasi ya kushiriki tushiriki kikamilifu," alisema.




Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Mhandisi Robert Gabriel (wa pili kulia), akikabidhi mashine ya kukata aluminium kwa mwanafunzi Manyama Yusuph aliyehitimu fani hiyo, wakati wa kukabidhi vifaa vyenye thamani ya Sh. milioni 98.78 kwa wahitimu 411 wa fani mbalimbali wa chuo cha VETA Mwanza, vilivyotolewa na Shirika la Plan International kwa ufadhili wa Umoja wa Ulaya kupitia mradi wa Vuka, juzi. **PICHA: ELIZABETH FAUSTINE**

# SGA yapata tuzo ya juu maonyesho ya madini

**Na Mwandishi Wetu,** GEITA

KAMPUNI ya ulinzi ya SGA Security imepongezwa kwa maendeleo yake ya kiteknolojia katika kutekeleza majukumu yake yaliyoiwezesha kushinda tuzo kwenye maonyesho ya nne ya teknolojia kwenye Sekta ya Madini yaliyofanyika mkoani Geita hivi karibuni.

Katika maonyesho hayo ambayo yalifunguliwa rasmi na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa na kushirikisha kampuni zaidi ya 400 kutoka ndani na nje ya Tanzania, kampuni hiyo iliibuka mshindi katika kipengele cha teknolojia katika usafirishaji na usalama.

Akizungumzia mafanikio ya kampuni hiyo, Waziri wa Madini, Doto Biteko, alipongeza maendeleo yake ya kiteknolojia ambayo alisema ni ya miaka mingi na yamepelekea kampuni nyingi ya madini kuwa na imani nayo, hivyo kuingia nayo mikataba ya ulinzi.

"Nitoe wito kwa uongozi wa kampuni hii kuendelea kuwa na uhusiano mzuri na ushirikiano wa dhati na serikali katika kuhakikishia ulinzi na usalama wa madini yetu dhidi wale wenye nia mbaya", alisema.

Waziri Biteko aliishukuru kampuni huyo kwa kukubali kuwa moja wapo ya wadhamini wa maonyesho hayo ya kila mwaka na ambayo hushirikisha wadau wa sekta ya madini kutoka ndani ya nje ya nchi ambao hufanya maonyesho yanayohusiana na shughuli wanazofanya katika sekta hiyo.

Mkuu wa Mkoa wa Geita ambao ndiyo wenyeji wa maonyesho hayo, Rosemary Senyamule, alipongeza SGA kwa mafanikio hayo na kuwataka wachimbaji wadogo na wakubwa kutumia huduma za teknolojia ya hali ya juu katika nyanja za ulinzi zinazotolewa na kampuni hiyo.

"Kwa kushirikiana na kampuni ya SGA mtajihakikishia ufanisi zaidi na ulinzi wa kutosha wa mali zenu hata kama hamtakuwa ameneo ya ofisi zenu na machimboni", alisema na kuongeza kampuni nyingine hazina budi kuiga mfano wa SGA," alisema.

Makamu wa Rais wa Mgodi wa Dhahabu wa Geita (GGML), Simon Shayo, alipongeza SGA kwa kuwekeza kwenye teknolojia ya ulinzi.

"Wengine wanadhani suala la ulinzi ni la mlinzi aliyebeba rungu au silaha nyingine, la hasha kuna zaidi ya hayo; SGA imewekeza kwenye teknolojia ya kisasa katika ulinzi jambo linalowatofautisha na kampuni nyingine", alisema.

SGA Tanzania, Eric Sambu, alibainishwa kufurahishwa kwake kutokana na mafanikio ya kampuni hiyo kutambuliwa na wadau mbalimbali ikiwamo Serikali, mafanikio ambayo alisema walistahili kuyapata kutokana na kujituma kwa wafanyakazi wa kampuni hiyo.

Aliwapongeza wafanyakazi wa kampuni hiyo kwa kuonyesha uwezo na mafanikio ya kiteknolojia ya kampuni hiyo ya ulinzi ambayo alisema huwapa wateja wake thamani halisi ya huduma wanazolipia ili kuzipata.

SGA ni kampuni kongwe ya ulinzi nchini iliyoanzishwa mwaka 1984, ikijulikana kama Group 4 Security. Kwa sasa imeajiri wafanyakazi zaidi ya 5,000 nchi nzima.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hatua zichukuliwe dhidi ya madiwani waliopigana

**MOJA** ya matukio yaliyotawala katika vyombo vya habari wiki hii ni lile la madiwani wa viti maalum katika Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga, kutwangana makonde kwa kile kilichodaiwa ni deni la Sh. 40,000.

Katika taarifa hiyo, ilielezwa kwamba mmoja wa madiwani hao alikuwa akimdai mwenzake kiasi hicho cha fedha, hivyo akataka amlipe mara baada ya kumalizika kwa kikao cha baraza la madiwani.

Chanzo cha taarifa hiyo ni kwamba, diwani aliyekuwa akimdai mwenzake, alikataa mdeni wake huyo kulipiwa na madiwani wenzao waliokuwa katika kikao hicho, akiwamo Mbunge wa Kahama, Jumanne Kishimba.

Mdaiwa huyo, inadaiwa kuwa alimwambia mdai wake kwa wakati huo hakuwa na pesa ya kulipa deni hilo, hivyo akamsihi waende benki ili akamlipe lakini aligoma na madiwani wengine walipotaka wamlipe kwa niaba yake, aligoma pia na kuanza kumpa kichapo diwani mwenzake.

Kwa ujumla, kitendo hicho kimetoa picha mbaya na hata baadhi ya wachambuzi wa masuala ya kisiasa na kijamii kwenda mbali zaidi na kueleza kuwa ugomvi baina ya madiwani hao ulikuwa zaidi ya deni linalodaiwa kuwa chanzo.

Hata hivyo, ni faraja kusikia kwamba suala hilo limeshafikishwa katika ofisi ya Meya wa Manispaa, Yahaya Bundala, ambaye alikaririwa na vyombo vya habari akisema wahusika wataitwa katika kamati ya maadili ya madiwani na hatimaye kuchukua hatua baada ya kupata ukweli.

Pamoja na taarifa kwamba watafikishwa katika vyombo vya nidhamu, ni vyema pia Chama Cha Mapinduzi (CCM) ambacho madiwani hao wanatokana nacho, kikachukua hatua kwa viongozi wenye heshima katika jamii kupigana hadharani na kutoa taswira mbaya na kuonyesha wazi kukosa maadili ya kichama na kiongozi.

Pia kabla ya kuchukua hatua, CCM inapasa kutoa tamko la kukemea kitendo hicho ambacho si tu kimesababisha taharuki miongoni mwa wananchi bali kukidhalilisha hicho tawala.


Kwa kawaida, kiongozi anapaswa kuwa mfano kwa kauli na matendo ili kulinda heshima yake na ya chama kilichomwamini pamoja na jamii anayoiongoza, hivyo kitendo cha madiwani hao kimewadhalilisha na jamii kukosa imani dhidi yao.

Miaka ya 1990, aliyekuwa mkuu wa wilaya katika wilaya mojawapo nchini, alidaiwa kupigana na mwananchi wakiwa katika baa kwa kile kilichodaiwa ni kugombani mwanamke. Hatua hiyo ilisababisha aliyekuwa Rais wa wakati huo, Mzee Ali Hassan Mwinyi, kutengua uteuzi wake mara moja.

Kadhalika, wakati wa serikali ya awamu ya tano chini ya Hayati Rais John Magufuli, aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Magesa Mulongo, aliripotiwa kupigana hadharani na aliyekuwa Katibu Tawala wa Mkoa huo, Dk. Feisal Issa. Baada ya taarifa hizo, Rais alitangaza kumtimua Dk. Issa huku Mulongo akihamishiwa mkoa mwingine.

Kwa mifano hiyo, ni matumaini kwamba hatua zitachukuliwa dhidi ya madiwani hao ili kulinda heshima ya chama, taasisi wanayoitumikia pamoja na kuonyesha umuhimu wa maadili kwa viongozi wawapo ndani na nje ya majukumu yao.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Bodi ya DAWASA isaidie kumaliza kero hii

**MAMLAKA** ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) ni miongoni mwa taasisi zenye tija kwa umma, ambayo inapunguza kero za upatikanaji wa huduma hiyo muhimu kwa wananchi.

Inatajwa mageuzi mengi yamefanyika kwenye sekta ya maji Mkoa wa Dar es Salaam, baada ya kuunganisha iliyokuwa DAWASCO na DAWASA, na sasa inatajwa kuwa miongoni mwa taasisi ambazo serikali inajivunia.

Ni kweli DAWASA inafanya kazi nzuri, lakini ninadhani bado ipo haja ya kuongeza kasi ili kuhakikisha maeneo yote ya Dar es Salaam yanapata huduma hiyo bila kikwazo chochote.

Watu kuunganishwa huduma hiyo bado kuna sintofahamu kwenye baadhi ya maeneo, hali inayosababisha wengine kukata tamaa na kudhani kwamba kuunganishiwa maji ni mchakato mgumu.

Badala yake maji wanayotumia ni yale yanayotembezwa na magari yakiuzwa lita 1,000 kwa Sh. 15,000, bei ambayo kiuhalisia ni kubwa ikilinganishwa na ya DAWASA ambayo lita hizo huenda bei yake isizidi Sh. 2,000.

Wakati mwingine maeneo ambayo watu hawajaunganishiwa huduma hiyo, inawezekana bomba la maji lilipitishwa kwenda kwingine, ikitokea limepasuka, maji yanaweza kumwagika hata mwezi mzima bila kukarabatiwa.

Matokeo yake ni watu kwenda kukinga maji hayo bila kutoa taarifa kwa mamlaka husika kuhusu ubovu wa bomba, kwani kupasuka huwa ni bahati nzuri kwao kwa kuwa wanapata maji ya bure.

Ninaamini kwamba kama wangekuwa na huduma hiyo, ingekuwa ni rahisi kutoa taarifa wanapoona tatizo hilo, lakini kwa sababu hawaipati, wanaona hiyo ndiyo nafasi kwao ya kupunguza gharama za kununua maji.

Sasa kwa kuwa DAWASA ina Bodi ya wakurugenzi, ni vyema ikafuatilia matatizo hayo ya kuyatafutia ufumbuzi wa kudumu, ili wananchi wanapohitaji kuunganishiwa maji wasipate usumbufu.

Pamoja na hayo, mabomba yanapoharibika, basi wawe tayari kutoa taarifa ya ubovu sehemu husika ili ukarabati ufanyike haraka, kuliko ilivyo sasa ambapo maji yamekuwa yakimwagika chini bila hatua zozote kuchukuliwa.

Mfano mmojawapo ni Malamba Mawili Kwa Ndodi ambako bomba limepusika muda mrefu wakaja mafundi wa DAWASA wakalifunga, likaharibika tena, na sasa linaendelea kumwaga maji chini.

Watu hawatoi taarifa na huenda wafanya hivyo kwa sababu hiyo ni nafasi ya pakee kupata maji hayo ambayo huuziwa lita 1,000 kwa shilingi 15,000 kutokana na kwamba eneo hilo ni watu wachache wenye mabomba ya maji.

Kwa kuwa bodi hiyo ni kiungo muhimu chenye majukumu mbalimbali yenye lengo la kufuata mbinu za kibiashara, sheria, taratibu na kusimamia taratibu za kazi na kutambua hatari zinazoikabili miradi ni vyema iyaone hayo.

Nitambua kuwa jukumu lingine la bodi ni kusimamia kwa umakini utawala bora na miongozo ili kuhakikisha huduma zinazohitajika kwenye umma zinatolewa inavyotakiwa tena kwa uadilifu.

Lakini pia kwa kuwa bodi ina jukumu la husimamia mahusiano mazuri na wadau wote kama njia mojawapo ya kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya kila siku, inaweza kumaliza kero za maji kwa wananchi.

Kimsingi, ili ni suala la utashi wa kisiasa ambao unaweza kusaidia DAWASA kufanya kazi bila kuwapo kero ambazo zimekuwa zikilalamikiwa na wananchi kila mara, hasa ukosefu wa huduma ya uhakika ya maji.

Vilevile itapendeza iwapo watu watahitaji kuunganishiwa huduma hiyo wakaipata bila mizunguko ambayo wamekuwa wakidai kukutana nayo na kusababisha wakate tamaa.

Kutokuwapo kwa uamuzi wa kisiasa ni njia mojawapo itakayosaidia kupunguza kama si kumaliza kero kwenye huduma hiyo muhimu kwa Watanzania ambayo baadhi yao wanadai kuisotea.

Mbali na kero hizo ipo nyingine ya lugha chafu za baadhi ya watumishi wa mamlaka hiyo kwa wateja wanapokwenda kufuatilia huduma, hali inayoweza kuharibu sifa nzuri ya DAWASA.

**SAFU**

## KWA MASLAHI YA TAIFA

# Elimu ya uzalendo ni muhimu kuelekea miaka 60 ya Uhuru



**Na Pascal Mayalla**

TUNAPOELEKEA kwenye maadhimisho ya Miaka 60 ya Uhuru na Jamhuri, Desemba 9, mwaka huu, Watanzania bado wanapaswa kufundishwa elimu ya uraia, tena si wananchi tu wa kawaida, bali hata baadhi ya viongozi wetu. Ni aibu kwa kiongozi mkubwa serikalini, yumo ndani ya serikali, halafu anaubeza Muungano. Anapotosha kuhusu muungano, anamaanisha nini?

Nimebahatika kusoma elimu ya msingi na sekondari enzi za Mwalimu Nyerere. Moja ya masomo mazuri sana na yalikuwa yanafundisha sana uzalendo ni Siasa. Enzi hizo mtu ukimaliza sekondari, hasa kidato cha sita, ilikuwa lazima ujiunge na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kwa mwaka mmoja kwa mujibu wa sheria. Baada ya hapo ndipo unaendelea na masomo ya vyuo ikiwemo Chuo Kikuu, hivyo taifa kupata viongozi wazalendo wa ukweli na uzalendo wao ni uzalendo wa kwelikweli.

Baada ya nchi yetu kuanza mfumo wa vyama vingi mwaka 1992, mambo mengi yalibadilika. Somo la siasa liliacha kufundishwa na badala yake likaanzishwa somo la elimu ya uraia. Hivyo, tunapoelekea kwenye miaka 60 ya Uhuru, somo la elimu ya uraia, linahitajika sana hasa kwa viongozi wetu ili kujenga kada ya viongozi wazalendo wa kweli wa nchi yetu.

Ninasema hivyo kwa sababu, ni ukweli kwamba katika hawa viongozi wetu tulio nao, baadhi si viongozi bali wachumia matumbo tu. Hawana uzalendo kabisa kwa nchi yetu na wengine ni viongozi mamluki waliovalia ngozi ya kondoo kwa nje lakini kwa ndani ni chui wala mbuzi!

Hivi karibuni nilikuwa nikiangalia mahojiano kwenye kituo kimoja cha televisheni nchini. Mmoja wa viongozi wetu wakuu wa kitaifa, kati ya wale viongozi wakuu sita wa kitaifa wanaotembea na ving'ora, alikuwa anahojiwa.

Katika maelezo yake, kiongozi huyo aliuzungumzia Muungano wetu adhimu si tu kwa hali kama ya kubeza, bali pia kwa kupotosha kuwa siku Tanganyika na Zanzibar zilipoungana, ni taifa moja tuu la Zanzibar ndilo lilipoteza utaifa wake, yaani 'sovereignty' na Tanganyika haikupoteza utaifa wake bali ilibadili tu jina kutoka Tanganyika kuwa Tanzania. Jambo hilo ni upotoshaji wa hali ya juu.

Sasa kama baadhi ya viongozi wetu hawa ndio hawaujui Muungano, tutegemee nini kwa watu wa kawaida? Elimu ya historia ya uhuru inahitajika sana kwa viongozi vijana wa kileo ambao wanaukwaa uongozi mkubwa huku hawajakomaa kiuzalendo.

Ukweli wa Muungano wetu ni wa nchi huru mbili, Jamhuri ya Tanganyika na Jamhuri ya Watu wa Zanzibar. Nchi hizi zote mbili zilipoteza utaifa kwa kuungana na ziliungana kwa muungano wa 'union'. Maana yake ni kuunganisha vitu viwili kuwa kitu kimoja na kuunda taifa jipya na Jamhuri mpya ambayo ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Zanzibar ilipoteza utaifa wake na kuukabidhi kwa Tanzania na Tanganyika ilipoteza utaifa wake na kuukabidhi kwa Tanzania, hivyo nchi zote mbili zilipoteza utaifa wao na kuunda nchi moja mpya ya Tanzania.

Dhima kuu ya Muungano wetu, kutoka kwa waasisi wetu, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Sheikh Abedi Amani Karume, ni udugu na umoja. Yaani kiasili kabisa ya ujio wa wageni nchini kwetu, sisi tulikuwa watu wamoja. Ukoloni ulipoingia Afrika, ndipo bara la Afrika likagawanywa kwa wakoloni katika ule mkutano wa Berlin wa mwaka 1884 ulioitishwa na kiongozi wa Ujerumani wakati huo, Chancellor Bismarck. Bara la Afrika likagawanywa ndipo tukawekewa mipaka ya wakoloni.

Katika mgawo huo, Tanganyika iligawiwa kwa Wajerumani na kuwa 'German East Africa' Kenya ilikuwa 'British Colony', wakati Zanzibar na Uganda zilikuwa 'British Protectorate', Zanzibar iligawiwa kwa Sultani wa Zanzibar na Uganda chini ya ufalme wa Kabaka.

Wakati huo milki ya Sultani wa Zanzibar, ilitapakaa hadi eneo la maili 10 za ukanda wa pwani ya Afrika Mashariki. Ujerumani na Uingereza zikaingia makubaliano ya kubadilishana maeneo katika mkataba wa Hellingoland ambapo Mjerumani alimpa aneo Mwingereza na Mwingereza akaliachia eneo la maili 10 za ukanda wa pwani.

Baada ya Vita Kuu vya Kwanza vya Dunia mwaka 1914-1918, Ujerumani ilishindwa vita, hivyo ikanyanganywa makoloni yake yote ikiwamo Tanganyika na kukabidhiwa kwa Mwingereza siyo kuwa koloni bali 'Trusted Colony' kwa ajili ya kuliandaa kujitawala.

Wakati wa harakati za uhuru miaka ya 1960, ukiwamo mwamko wa umajumui wa Afrika (Pan Africanism) ulioasisiwa na Kwame Nkurumah wa Ghana, Mwalimu Nyerere alikuwa tayari kuuchelewesha uhuru wa Tanganyika ili kuwasubiri majirani zetu Zanzibar, Kenya na Uganda ili tupate uhuru pamoja na kuziunganisha nchi zetu ziwe taifa moja.

Sijui nini kilitokea hili likashindikana lakini Tanganyika ikapata uhuru wake Desemba 9, 1961 na Zanzibar ikapata uhuru wake (wa bandia) Desemba 10, 1963. Baada ya mwezi mmoja ndipo kukafanyika yale Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ya Januari 12, 1964.

Baada ya hapo, Karume alizungumza na Nyerere, kisha Muungano wetu adhimu akaasisiwa kwa dhima tu kuwa sisi ni ndugu, sisi ni wamoja. Ndani ya Muungano hakuna sisi wala wale. Sote sisi ni Watanzania, hivyo ni jambo la ajabu sana anapoibuka kiongozi wa serikali na kuanza kuleta hoja za sisi na wale.

**pascomayalla@gmail.com**
**0754 270403**

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Mzee wa Mvomero na madadapoa kazi ipo



**Na Joseph Kulangwa**

MKUU wangu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makala, asalaam aleykum! Mzee wangu kaniomba nikwambie haya yafuatayo, ambayo anaamini yatakusaidia katika safari yako ya kuongoza jiji hili lenye mambo mengi.

Anasema umeanza vizuri sana kushughulikia ustawi wa jiji hili ambalo hakika unalifahamu na umeliishi kwa muda mrefu mpaka ukawa alwatan, ukiimbwa na baadhi ya bendi wakikuita pedejee, Mzee wa Mvomero!

Uliimbwa si kwa mabaya bali kwa wema wako uliokuwa nao kwa jamii, hususan vijana, ukijua matatizo yao ya kiuchumi na kijamii, lakini pia kisiasa ukipata kuwa kiongozi ndani ya Umoja wa Vijana wa CCM, tena wakati huo usibague hawa wa chama tawala na hawa wa upinzani.

Anasema hakika Chifu Hangaya hakufanya makosa kukurejesha Dar es Salaam, ulikokulia mpaka vijana kukuita Mzee wa Mvomero, lakini ukiwa ni mmoja wao. Bila shaka jiji utaliweza.

Ulianza na vijana wetu wafanyabiashara wadogo, wajasiriamali waliobatizwa jina la Wamachinga kutokana na maneno ya Kiingereza ya Marching guys, wakianza enzi hizo kwa kuchuuza bidhaa zao mitaani wakitembea.

Lakini siku zilivyosonga wakajikita na kujisimika katikati ya Jiji tena milangoni mwa maduka ya wafanyabiashara wakubwa na kuzua kilio na malalamiko na hatimaye ukaja hivi karibuni na suluhisho.

Kilio na malalamiko haya, vilikuwapo na bila shaka vingeendelea kama awamu ya tano ingeendelea, vingeendelea kama Chifu Hangaya asingekurejesha jijini Dar na kukupa nafasi hiyo.

Ni dhahiri, kazi inaendelea kwa sababu Wamachinga bado hawajapata mahali pa kudumu pa kuendesha biashara zao, mahali ambako bila shaka watapata wateja kama waliokuwa wanawapata Kariakoo.

Mzee wangu huyu anashangaa kwamba kabla hilo halijakamilika, umeingia kwa dada zetu hawa wanaopachikwa majina lukuki ya machangudoa, madadapoa mara makahaba, mara malaya huku wao wakijiona ni wajasiriamali kama walivyo Wamachinga.

Wakidhani kuwa huenda siku moja utakuja na suluhisho la kuwatengea maeneo ili nao wawe wajasiriamali kama wengine. Mzee anasema ungejikita kwanza katika suala la Wamachinga, limalizike ndipo uanze mengine.

Anasema alikuwapo mtangulizi wako hapa ambaye kila kukicha alikuwa na jambo lake. Mara watoto telekezwa, ndoa telekezwa, mimba telekezwa na kadhalika, lakini akaishia kusikojulikana.

Kwamba alikuwa akishika hili, kabla halijamalizika anahamia lingine, mara walimu wasilipe nauli za daladala, kana kwamba ndiyo kada pekee inayolipwa kichele, na kusahau kuwa kuna watu jijini hapa kwao mlo mmoja ni shida.

Akisahau kuwa mitaani kuna watu hawana ajira kila leo ni kama jana na hawajui kesho yao. Lakini hawakuwa na msamaha wa daladala au hata tiba, kila kitu pesa ambayo imeota matairi.

Mzee anasema suala la hao wanaoitwa changudoa, halikuanza leo, ni la enzi na enzi ni la karne na karne hata kwenye Biblia limo, limetamkwa. Walikuja watu Dar es Salaam wakalipigia kelele lakini wakagonga mwamba.

Kuna mkoa gani nchini ambako tangu enzi za Mwalimu Nyerere haukuwa na mtaa maarufu wa hao kina dada, tena wakitoka mkoa mmoja wa Kaskazini, wakiwa maarufu kwa kutoza shilingi mbili na kuishi gizani vibandani wakimulikwa na vibatari?

Nyerere hakuwaondoa, Ali Hassan Mwinyi hakuwaondoa, akaja Ben Mkapa akawaacha tu, akaingia Jakaya Kikwete hakuna kitu, akaingia John Magufuli halikadhalika wapo tu.

Hivi ndugu yangu Makala, utawaondoaje wakati wateja wapo? Tena wateja wengine ni wa kada yako ambao wakisikia juhudi zako za kutaka kutumia polisi kuwaondoa, wanakucheka jino pembe!

Mzee anakuhadharisha kuwa usije ukawa unatwanga maji kwenye kinu yakakumwagikia bure na kukuchafua. Shughulikia jambo moja ambalo ni gumu kidogo la Wamachinga hawa ambao wakikosa cha kufanya watahatarisha maisha ya raia na mali zao.

Hawa dada zetu masikini sidhani kama wana hata uwezo wa kushika silaha za kuvunja majumba na kuiba tofauti na Wamachinga ambao wengi wao ni midume. Ukiweza watafutie na wao utaratibu tu wa kistaarabu waendelee na fursa yao na kulipa kodi.

Itakuwa ngumu sana kuwaondoa huku huna mbadala wa kuwaendeleza kimaisha. Na tena afadhali hao wanaojionesha kuliko wanaojificha kwenye ajira na kuyafanya hayo. Wateja wao wanakuangalia tu ujikwae.

**Alamsiki!**

## KONA YA UKWELI

# RC Makalla unajua kwa nini maagizo hayatekelezwi na watendaji wako?



Na Thobias Mwanakatwe

RAIS Samia Suluhu Hassani, Mei 15, mwaka huu, alifanya uteuzi wa wakuu wa mikoa huku akimteua Amos Makalla kuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam kuchukua nafasi ya Aboubakar Kunenge ambaye alihamishiwa Mkoa wa Pwani kuchukua nafasi ya Evarist Ndikilo ambaye amestaafu.

Uteuzi wa Makalla ambao unatajwa kuwa na changamoto nyingi hasa kutokana na ukubwa wake pamoja na kuwapo kwa idadi kubwa ya watu kutoka ndani na nje ya nchi, ulipokewa vizuri na wananchi hasa kutokana na uzoefu wake wa kushika wadhifa huo katika mikoa mbalimbali.

Nampongeza sana Makalla kwa kuwa kazi anayoifanya ni nzuri kujaribu kuzikabili changamoto kadhaa jijini Dar es Salaam ambao ni mji wa kibiashara.

Pamoja na utendaji wake mzuri, nachelea kusema asipokuwa mkali kwa watendaji walio chini yake atakwama. Dalili hizo nimeanza kuziona kutokana na maagizo anayoyatoa mara kadhaa.

Kama kumbukumbu zangu zipo sawa, hata aliyewahi kuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, alishawahi kulalamika sana kukwamishwa na watendaji walioko chini yake katika utekelezaji wa miradi ndani ya mkoa huo.

“Watendaji wenzangu jana ilikuwa aibu, jana nimedhalilika mimi. Watendaji wangu jana mmenivua nguo na aibu ile imenifanya hata sijalala, usingizi sijaupata kabisa mpaka nikawa najiuliza mimi nakosea wapi kwa sababu tunakaa vikao vingi vya kutoa maelekezo mengi dhidi ya miradi ya maendeleo katika mikoa wetu lakini hakuna kinachofanyika,” alisema.

Maelezo hayo ya Makonda yalionyesha dhahiri kuwa kuna tatizo la watendaji katika mkoa wa Dar es Salaam kwa kutotekeleza maagizo na maelekezo wanayoopewa na wakubwa wao. Hali hii ndiyo inazorotesha maendeleo katika mkoa.

Kilichokuwa kikimpata Makonda ndicho hicho ninachoanza kukiona kwa Makalla ambaye kila maagizo anayoyatoa kwa watendaji wake, naona hayatekelezwi ipasavyo. Mimi pis nikiwa mkazi wa Dar es Salaam, lazima nilisemea hili gonjwa la watendaji.

Nitatoa mifano michache. RC Makalla Julai, mwaka huu, aliitisha kikao cha Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa kupitia tathmini ya utekelezaji wa mwongozo uliotolewa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto juu ya kujikinga na corona na kutoa maelekezo ya suala la ‘level seat’ na uvaaji wa barakoa.

Makalla aliagiza kila abiria anayepanda kwenye vyombo vya usafiri kuvaa barakoa huku akiwataka wamiliki wa vyombo hivyo kuwaelekeza madereva na makondakta kuepuka kubeba abiria asiyevaa barakoa.

Makalla katika kuhakikisha maagizo hayo yanatekelezwa na kuzingatiwa, alitoa maelekezo kwa Jeshi la Polisi, Wakuu wa Wilaya na Mamlaka ya Udhibiti wa Usarifi wa Ardhini (LATRA) kuhakikisha wanasimamia ipasavyo mwongozo wa Wizara ya Afya.

Kutokana na changamoto za usafiri kwa wanafunzi, RC Makalla aliruhusu daladala kubeba wanafunzi watano watakaosimama lakini kwa kigezo cha wanafunzi hao kuwa wamevaa barakoa.

Siku tatu baada ya maagizo hayo, nilifanya utafiti kuangalia kama agizo la kutaka abiria wanaopanda daladala wanavaa barakoa linazingatiwa. Nililazimika kupanda daladala kutoka Mwenge kwenda Gongo la Mboto na katika gari nililopanda, abiria waliokuwa wamevaa barakoa ni watatu tu nikiwamo mimi wengine zaidi ya 20 wakiwa hawajavaa.

Nikaona hiyo haitoshi, nikapanda daladala kutoka Gongo la Mboto kwenda Kivukoni. Hali ikawa hiyo hiyo. Hadi sasa utekelezaji wa agizo la RC Dar umefeli kwa sababu watendaji waliotakiwa kusimamia agizo hilo hawajaifanya kazi hiyo ipasavyo.

Lakini wakati nikiendelea kutafakari ni kwa nini agizo hilo la RC halijasimamiwa ipasavyo na watendaji ilihali Dar es Salaam ina hatari kubwa kupata maambukizi ya corona, nimeshtuka baada ya kuona Makalla anakuja na agizo lingine jipya .

Sina uhakika kama agizo lile la abiria kutakiwa kuvaa barakoa kila wanapopanda magari hayo alifanya tathimini kujua kama lilifanikiwa kwa kiasi gani.

Katika agizo lake jipya, Makalla amelielekeza Jeshi la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam kuanza msako wa kuwabaini wezi wa vifaa vya magari, vibaka, kuwakamata na kuwachukulia hatua kali za kisheria.

Alitoa agizo hilo wiki iliyopita wakati wa kikao cha tathimini ya ziara yake ya kusikiliza migogoro jimbo kwa jimbo.

Alisema kumeanza kuibuka vitendo vya wizi na kuleta taharuki kwa wananchi jambo ambalo hawezi kulifumbia macho.

Binafsi niliposikia agizo hilo nilifurahi sana maana katika mambo yanayokera sana hivi sasa katika Mkoa wa Dar es Salaam ni kuibuka kwa kasi wizi wa vifaa vya kwenye magari.

Wizi huo ambao wakati wa serikali ya awamu ya tano ulikwisha kabisa, hivi sasa ukiwa na gari lako unapolipaki sehemu yoyote hata kama ni kwa muda mfupi unakuwa na wasiwasi kwa sababu wezi wa vifaa vya magari wamekuwa wengi karibu kila mtaa.

Makalla ana nia njema ya kutaka kuhakikisha Dar es Salaam inakuwa na hali ya amani kama ilivyokuwa. Lakini hofu yangu ni je, agizo lake hilo kwa watendaji wake litatekelezwa au litapotezewa kama suala la uvaaji barakoa kwenye daladala?

Ni vyema mkuu wangu wa mkoa asiache kufanye tathimini kuona kama maagizo anayoyatoa yanafanyiwa kazi na watendaji walioko chini yake au yanawekwa kapuni.

**Kwa moani na ushauri tumia barua pepe mwanakatwe2015@gmail.com**

## DARASA LA NDOA

# UBAKAJI NA UNG’ANG’ANIZI KATIKA NDOA



Na Mch.Dk. Enock Mlyuka

UBAKAJI na ung’ang’anizi wowote husababisha hofu ambayo inasitisha hisia za kimapenzi kwa mwenzi. Kufanya tendo la ndoa bila ridhaa na utayari wa mwenzi ni ubakaji katika ndoa. Hali hii humfanya mwenzi awe na maumivu makali wakati wa tendo la ndoa, hasa kwa upande wa mwanamke.

Kufanya hivyo ni dhuluma dhidi ya mwenzi. Anayevamiwa hawezi kulifurahia tendo hilo kwa namna yoyote ile. Huu ni ubakaji na matokeo yake ni kuanza kufikiria kushawishika na kule anakoweza kufurahia tendo hilo. Hapa ndipo hukaribishwa wale watu wanaoitwa “Serengeti boys”, “Sugar Mummy” na “Sugar daddy” au vidumu.

**Kama mume huyo anakutana na tabasamu, kauli njema, ukaribisho mzuri wenye bashasha toka kwa mhudumu wa hoteli wakati nyumbani kwake ni mambo adimu kuyapata, hali hii huwa ni jaribu kubwa kwa bwana.**

Yanayosemwa juu ya mwanamke yanaweza kusemwa vile vile juu ya mwanamume. Ikiwa mume anakuja nyumbani, mapokezi ni baridi, hakuna lugha na matendo yanayohamasisha na kuchochea nguvu ya matendo na mapenzi, basi mwanamke anaweza kumtumia mumewe kama chombo. Kama mume huyo anakutana na tabasamu, kauli njema, ukaribisho mzuri wenye bashasha toka kwa mhudumu wa hoteli wakati nyumbani kwake ni mambo adimu kuyapata, hali hii huwa ni jaribu kubwa kwa bwana huyo.

Maswali ya msingi ya kujiuliza ni haya: Je, mwenzi aliyechoka kwa sababu ya majukumu ya kikazi akifika nyumbani anakuta mapokezi ya aina gani? Lugha ikoje? Akifika nyumbani hali ikoje? Kwa nini unatafuta vivuruge wa ndoa yako wakati wewe mwenyewe ni mvurugaji namba moja?

Wako wanandoa ambao hawapendi kurudi nyumbani mapema kwa sababu ya mazingira yasiyovutia ya nyumbani. Nyumba kwa baadhi ya wanandoa imegeuka kuwa gereza na jehenamu kwa sababu wanandoa wamepoteza mvuto dhidi yao. Nyumba umekuwa uwanja wa mapambano dhidi yao badala ya kuwa chimbuko la amani, umoja, mshikamano na maadili mema. Wanandoa wanapaswa kuona thamani na umuhimu wa uwepo wao. Thamani na umuhimu wa mwanandoa kwa mwenzi wake anautengeneza mwenyewe.

Kuanzisha uhusiano nje ya ndoa kama njia ya kutafuta suluhu ya tatizo ni kukoseana haki kwa wanandoa, watoto na kuhatarisha uhai wa ndoa na familia. Kila mwanadamu ameumbwa ili apendwe. Hitaji hili ni kubwa zaidi kwa upande wa wananawake kuliko wanaume. Kiu kubwa ya mwanamke yeyote ni kupendwa na mume wake.

Hata hivyo ni muhimu kufahamu kuwa upendo hauji hivi hivi bali hutengenezwa kwa kauli na matendo mema ya mwenzi. Upendo unahitaji kuwajibika na kujirudi. Wanandoa wajifunze kutendeana na kuneneana mema katika maisha yao ili kumsha hisia za upendo siku zote za maisha yao.

Mpende mwenzi wako na kama huwezi kumridhisha kwa mapendo, basi usimjeruhi kwa vituko vyako. Baki njia kuu, mchepuko siyo dili. Ndoa pasipo upendo ni changamoto kubwa.

Kinyume cha hapo ndoa inaweza kuwa chimbuko la mateso, maumivu, uonevu, kutumiana, kuhujumiana na kudanganyana. Hali hii ni kinyume cha sheria na makuzi ya mume na mke. Ndoa kati ya mume na mke, inaendana na kile alichoratibisha Mungu alipomuumba mwanamume na mwanamke, akiwataka waungane na kuwa mwili mmoja.

Katika ndoa ni lazima kuwe na mawasiliano na makubaliano baina ya mume na mke ili wote wawe na furaha, amani na upendo. Asili ya ndoa ni Mungu na alitaka kuwapo na furaha badala ya mateso. Lengo kuu ni kuleta uhusiano mzuri wa kupendeza ili kuboresha maisha ya wanandoa.

Ndoa ni kujifunza. Hakuna anayezaliwa anajua kila kitu. Yapo mambo ambayo mwanamke anayajua, lakini mwanamume hayajui. Vile vile kuna mambo mwanamume anayajua lakini mwanamke hayajui. Kwa hiyo wanandoa wanahitaji zaidi mazungumzo na mawasiliano ili kupeana mawazo huru kwa upole na upendo ili kuifanya ndoa kuwa la furaha na mvuto.

Ndoa ni furaha. Furaha ya maisha ya ndoa ni jukumu la wanandoa wote wawili. Ni jambo ambalo halina budi kujenga uhusiano wa karibu (intimancy) na ulio bora wa wanandoa. Lengo kuu la wanandoa ni kuishi maisha ya furaha. Wanandoa wote wawili wanapaswa kufurahia maisha ya ndoa, kila mmoja kuridhika na mwenzi wake na kumtukuza Mungu.

**■ Dk. Mlyuka ni mchungaji wa KKKT na Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare), asasi inayojishuhulisha na masuala ya ndoa, familia na malezi. Kwa maelezo zaidi, tembelea www.tamcare.or.tz. Fuatilia mafunzo zaidi katika tamcaretv online. Kwa maoni na ushauri wasiliana naye kwa: info@tamcare.or.tz au +255744000066.**

**Asili ya ndoa ni Mungu na alitaka kuwapo na furaha badala ya mateso. Lengo kuu ni kuleta uhusiano mzuri wa kupendeza ili kuboresha maisha ya wanandoa.**

OKTOBA 3, 2021
Nipashe

# MAISHA

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*



Ukurasa 14

**Kunywa juisi ya moto**



Ukurasa 15

**MAISHA NI NYUMBA**

Jinsi ya kupangilia chumba cha mtoto wa kiume



**HARUSI**

Ukurasa 12




**MIGUU INAYOSEMA**

## Limao, asali inakupa jibu sahihi

Ukurasa 14


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA






| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ■ | S | H | I | D | A |
| ■ | H | ■ | ■ | A | ■ |
| D | A | U | ■ | W | ■ |
| ■ | M | ■ | J | A | A |
| ■ | B | ■ | ■ | T | ■ |
| B | A | N | G | I | ■ |


## AMSHA AKILI




## TOA TOFAUTI 5




## FUMBO TOTO




Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi:
LIA, VAA, TAMBO, SHUKA, KILIMO, SHAMBA

## WATOTO

# PAKA RANGI




Alichokifanya daktari

MTOTO Daudi alikuwa akitembea na baba yake wakielekea sokoni, wakiwa njiani ghafla Daudi alianguka na kuumia kidole. Baba yake alimnyanyua na kuanza kumbembeleza kutokana na kilio cha uchungu.

**Baba:** Mwanangu pole, nyamaza basi

**Daudi:** Baba lakini mwalimu alinidanganya

**Baba:** Kwa nini tena, kwani kuanguka kwako kunamuhusu nini?

**Daudi:** Si alisema kujikwaa si kuanguka!

**Baba:** Hajamaanisha ukijikwaa huwezi kuanguka, bali ina maana kufanya kosa moja si mwisho maisha, lazima upigane.

**SWALI**

Mnyama twiga anakula chakula gani?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Nyenyekea urudi kwenye nafasi yako

***KARIBU tena msomaji wangu tuendelee na mada yetu kuhusu nafasi au cheo. Nimefululiza kidogo mada hii kutokana na umuhimu wake katika maisha yetu ya kila siku. Tayari nimeshaeleza kwa nini watu wanaondolewa nafasi zao iwe ni kazini au kwenye ndoa na kutoa mifano waliokumbana na kadhia hiyo.***

LEO nitajaribu kudodosa namna mtu anavyoweza kurudi kwenye nafasi yake. Yakupasa kuelewa kwamba kila mtu Mungu alimpa nafasi na kuna mahali alitaka uwepo. Lipo moja ya andiko lake kwamba: "akanitoa, akanipeleka panapo nafasi, aliniponya kwa sababu alipendezwa nami".

Hii ina maana kwamba kama unatolewa, lazima upelekwe kwenye nafasi. Unaposhuhudia umetolewa lazima tuone nafasi. Usipopelekwa nafasi nyingine baada ya kutolewa, tayari hilo ni anguko. Mungu huwa anakutengenezea nafasi kwani nafasi yako ndio baraka zako.

Kila mtu katika ulimwengu wa roho ana nafasi yake. Lakini wapo watu hawajui nafasi zao. Hata wale waliokuwa kwenye nafasi wakatolewa hadi leo wanashangaa mambo hayaendi vizuri. Unaposema "Mungu ameniinua", lazima tuone nafasi yako ni ipi na mafanikio yako ni yapi kwani vyote vinambatana.

Nafasi yako ni cheo chako. Cheo huanzia kwenye ulimwengu wa roho, kisha kudhihirika katika ulimwengu wa mwili tunaouona kwa macho yetu. Siku zote mtu huanza kuanguka kwenye ulimwengu wa roho (ule usioonekana).

Ukiona mtu anafukuzwa kazi, anafilisika, anaporomoka kiuchumi, ndoa inavunjika, vyote hivi vinaanzia kwenye ulimwengu wa roho kwani ndio unaoamua kuhusu nafasi yako. Ukishapandishwa cheo katika ulimwengu wa roho, hata kama watu wafanye vikao wakatae, hautabadilishwa.

Ukiona haupo kwenye nafasi yako ujue umeshatolewa. Mama mmoja akanipigia simu wiki iliyopita baada ya kusoma moja ya makala hizi akasema; "Mume wangu hayupo nyumbani miezi kadhaa sasa. Na nilipodadisi nimegundua yupo kwa mwanamke. Lazima ajitafakari kwa nini ameondoka?

Mama huyu alidhani ana mume kumbe mume jina. Kumbe tayari kashatolewa kwenye nafasi. Wapo wanaume wanalishwa na wake zao, hawachangii chochote. Hata hivyo, wanawake nao ni wa ajabu sana. Akimlisha mumewe mwezi mmoja anadai gharama.

Yupo mwanamke atanunuliwa nguo na mumewe kwa kuwa hana kazi. Lakini ngoja mwanamke huyu apate kazi, mwanamume atashangaa kwa vituko atakavyofanyiwa.

Wapo wanaume ambao hawapo kwenye nafasi zao kama baba wa familia; kwamba mimi naingia ulingoni nalipa ada za shule, nalipa kodi ya nyumba, lakini hawana uwezo. Mungu anapokupa nafasi, anakupa pia uwezo.

Ukiona uwezo wako unapotea, elewa kabisa umetolewa kwenye nafasi na huwezi kufanya kazi kwa ubora ule wa awali. Na mwanamke anapoona mume amemkimbia lazima ajipime na kujiuliza; "je, niko sawa kwenye nafasi yangu?"

Wanaume wengine ni waoga pale wanapoona mke anamdhibiti kwa kumkaripia na wakati mwingine kutawala majukumu yake kama baba wa familia. Mfano baba akiongea anabezwa na inapofikia hatua hiyo, mawazo ya baba ni rahisi sana kugawanyika.

Akitoka nje kujiliwaza kutokana na tafrani za nyumbani, akipata mfariji, hapo ndipo tatizo la kuipiga kisogo familia yake huanzia. Kisa mama kawa mkali, hamtii tena mumewe na ndicho chanzo cha kupoteza nafasi yake kama mama. Kwa kutojua, pia anampotezea baba nafasi ya kuiongoza familia.

Nini cha kufanya mtu aliyepoteza nafasi aweze kuirudisha? Yapo maeneo mengi ila leo nitaje moja. Unyenyekevu ni moja ya silaha muhimu kulinda nafasi yako ili ahadi ya Mungu udumu kwenye nafasi yako. Yeye hana mpango wa kukushusha bali kukupeleka juu zaidi.

Unyenyekevu ni moja ya silaha unayopaswa kuitumia kudumu na hata kurudishwa kwenye nafasi yako. Unyenyekevu ni ile hali ya kubadilika kutoka ndani ya moyo. Ni tabia ya kiungu ndani ya mtu.

Ukiona mwenzio amekengeuka, tumia unyenyekevu kumrudisha. Ukimjia juu, utampoteza. Hupaswi kujilinganisha na kiongozi wako. Ni muhimu uheshimu nafasi ya kiongozi wako. Kubali hata kudharauliwa kwani ipo neema ya Mungu itakutetea.

***Mpenzi msomaji, bila shaka lipo jambo umejifunza kuhusu siri iliyojificha cheo au nafasi ya mtu kuchukuliwa . Kama utakuwa na maoni au kisa cha kimaisha ungependa tujadili pamoja, tuma ujumbe mfupi kupitia 0715268581.***

## NAWAZA KWA SAUTI
Na Salome Kitomari



# Chanjo ya corona muhimu, vinginevyo tutapoteza wengi

MARA kadhaa viongozi wa serikali wametoa maelekezo ya namna ya kujikinga na corona ikiwa ni pamoja na namna ya kukaa ndani ya vyombo vya usafiri, uvaaji barakoa na kunawa mikono mara kwa mara, tena kwa sabuni na maji tiririka.

Ilifikia mahali kuwa usipovaa barakoa hutaruhusiwa kutumia chombo cha usafiri lakini kwa sasa hali ni kawaida kama vile corona haipo. Hali hiyo inaonyesha kuwa bado wananchi hawajaona umuhimu wa kuchukua tahadhari.

Mathalani, katika kituo cha mabasi cha Magufuli na vingine nchini, wasafiri na wasindikizaji wanaingia na kutoka katika kituo hivyo lakini bado hakuna tahadhari kubwa inayochukuliwa kwa kuwa hakuna utaratibu wa kulazimisha watu kuvaa barakoa.

Unapoingia kituoni unachoulizwa ni malipo ya kuingia basi lakini asilimia kubwa ya waliomo humo hawajavaa barakoa na hakuna vyombo vya kunawia mikono.

Utaratibu huo upo pia kwenye vituo vingine na maeneo yenye mikusanyiko kuanzia nyumba za ibada, sokoni, mnadani na kwingine, wengi wanaona corona imeisha na sasa kila mtu yuko huru kuishi kama hakuna ugonjwa.

Kwa sasa kuna chanjo na hamasa inaendelea ili wengi wa chanjwe kwa kuwa hadi sasa zaidi ya dozi milioni moja zilizopo nchini zilizotumika ni zaidi ya 400,000 pekee, jambo ambalo linaonyesha hamasa ya chanjo haipo miongoni mwa wanajamii ndiyo maana hawavai hata barakoa.

Watu wanaendelea na maisha utadhani corona haipo. Hata nje ya mabasi hakuna viakasa mikono wala abiria haulizwi kuhusu barakoa bali wanaingia ni kawaida kukuta wengi hawajavaa barakoa.

Hakuna ubishi kuwa corona ni tishio kwa sasa na watu wengi wameugua na wengine kupoteza maisha na husambaa zaidi kwenye vyombo vya usafiri ambako kuna mikusanyiko lakini bado hakuna tahadhari inayochukuliwa.

Maagizo ya viongozi mbalimbali kuwa ni lazima abiria au watu wanapokuwa kwenye mikusanyiko wavae barakoa yameishia hewani kwa kuwa hayana utekelezaji, jambo ambalo siyo sawa kwa kuwa ilipaswa kuwa na ufuatiliaji kuhakikisha kuwa watu wanajikinga na corona.

Nchi ambazo zimeruhusu mikusanyiko kwa sasa ni zile ambazo watu wake wameshachanjwa kwa maana ya kwamba nchi nzima wamechanjwa na wanahakikisha wanapokuwa kwenye mikusanyiko wanavaa barakoa. Wanatakasa mikono na yote hiyo ni kujikinga kwa kuwa hata mtu akichanja bado ana uwezekano wa kupata ugonjwa huo na hata kupoteza maisha.

Kwa nchi bado watu hawajachanja inavyotakiwa wachache wameamua kusikiliza ushauri wa wataalam na kuchanja lakini wengi wamebaki na msimamo wa kutochanja kwa sababu zao wenyewe.

Wataalam wamethibitisha kuwa mtu aliyechanja anakuwa ameongeza askari wa kumlinda mwilini na inapotokea mashambulizi yoyote askari wale hupambana na kuwa washindi, hivyo hata akipata corona haitamyumbisha au kugharimu maisha yake kama yule ambaye hajachanja.

Ni muhimu nguvu ikaelekezwa kuelimisha wananchi kuchanja kama ambavyo inafanyika kwa baadhi ya nyumba za ibada ambazo viongozi wake wameamua kuwa mfano kwa kuchanja hadharani na wengine wakitoa maelekezo kwa viongozi wengine wa kanisa hilo kufanya hivyo.

Ikifikia mahali Watanzania wote wenye umri wa kuchanja wakachanjwa, ndipo tutaweza kuwa salama kwa kuwa tutapambana na kirusi kwa urahisi zaidi. Lakini hali ikiendelea hivi na watu hawachukui tahadhari zote muhimu, kuna hatari ya kuendelea kupoteza watu wengi zaidi.

Mathalani, wapo ambao bado hawaamini kwamba corona ipo na inaua au watu wanaugua na kupata madhara ya muda mrefu kwenye mwili, lakini pia kuna gharama kubwa ya matibabu ambayo wakati mwingine familia zinashindwa kumudu.

Inashangaza mtu anakwenda hospitalini hajavaa barakoa na mara nyingi ni kwenye hospitali binafsi ambazo ni vigumu kulazimisha uvaaji wa barakoa, hakuna ubishi hospitalini kuna mengi ikiwamo corona lazima watu wajikinge lakini wapo ambao wanakwenda bila tahadhari yoyote jambo ambalo siyo sawa kabisa.

Ifike mahali kwamba huiingii kokote bila kuvaa barakoa, kutakasa mikono kwa sanitizer au kunawa kwa maji tiririka na sabuni, vinginevyo itachukua muda mrefu ugonjwa huu kupungua nguvu.

Kwa sasa ugonjwa umesambaa hadi vijijini na watu wanapoteza maisha, mbaya zaidi watu wanakwenda kwenye misiba na kukusanyika kama kawaida yaani wanaendeleza utamaduni wa kuomboleza kwa mikusanyiko kama kawaida, jambo ambalo halitakiwi.

Ni muhimu viongozi wa dini wa maeneo hayo kuhamasisha watu kuhakikisha wanavaa barakoa na kubadili taratibu za kuwafariji wafiwa, kwa kuwa unakuta mtu anajulikana kafa kwa corona lakini bado watu wataambatana kwa wingi na kumkumbatia au kumshika mfiwa,hata kama yeye hana anaweza kuambukizwa.

Ni muhimu kuchukua tahadhari kwa kuwa UVIKO-19 ipo na imeshakatisha maisha ya wengi na wengine wapo hospitalini wanatetea uhai wao.

***MUNGU IBARIKI TANZANIA***

# HARUSI









Septemba 30, mwaka huu, ilikuwa sherehe ya kumuaga (send-off) Dorice Tesha, iliofanyika mjini Musoma mkoani Mara na leo Jumapili anatarajia kufunga ndoa na Fred Yona, katika Kanisa la Wasabato lililoko kitongoji cha Bima, Buhare mjini humo. Tunawatakia maisha mema katika ndoa yao.

# MITINDO



# MWENDO WA BLEZA, JEANS

VAZI la koti lenye mwonekano maridadi maarufu kama 'Bleza' limepata umaarufu sehemu mbalimbali duniani.

Aina hii ya uvaaji imezidi kusambaa na kuwabamba vijana wengi, kutokana na nguo hizo kuwa rahisi na hazina upendeleo.

Bleza ni jina linalotumiwa kwa koti la suti inayovaliwa bila suruali yake, hivyo humfanya mtu kuwa na mwonekano wa kupendeza.

Kwa ujumla vazi hili linavaliwa na wanaume na wanawake, kwa sababu huleta mwonekano mzuri katika mazingira yote.

Hata hivyo, ukichanganya bleza na suruali ya Jeans ni maalum kwa vijana wa kileo kutokana mtindo huo kuwa maarufu karne hii.

Unapovaa Bleza na Jeans, ndani unaweza kuvaa fulana nyeupe ili kunakshi vyema taswira yako.

Miguuni ni chaguo lako tu, unaweza kuvaa raba, viatu vya ngozi, snika au viatu vya wazi.





UREMBO



MIGUU INAYOSEMA

# Limao, asali inakupa jibu sahihi

UREMBO wa mwili wa mwanamke ni jambo muhimu, hasa kwa kuwa na mwonekano murua.

Miguu ni kiungo muhimu kinachochangia uzuri wa mwanamke, lakini mara nyingi haiwekewi umuhimu kama ilivyo uso au sehemu nyingine.

Katika safu yetu ya leo, tutaelekeza namna ya kutunza ngozi ya miguu.

Wanawake wengi wamezoea kwenda saluni kwa ajili ya kusuguliwa miguu, bila kujua ni kazi rahisi ambayo mtu anaweza kuifanya akiwa nyumbani.

Urembo huu ni rahisi tena ni kwa gharama nafuu, unaweza kuupata nyumbani kwako tu na ukaonekana mwenye mvuto zaidi.

Mahitaji ya kusafisha miguu yako na ikaonekana maridadi ni limao, asali, maziwa mgando, mafuta ya mzaituni na mafuta ya nazi.

**NAMNA YA KUSAFISHA MIGUU**

Chukua limao lako, changanya na asali pamoja na mafuta ya mzaituni au chukua limao chovya kwenye asali na mafuta ya mzaituni, kisha anza kusugua miguu yako.

Baada ya kuisugua acha kwa muda wa dakika 10-20 kisha paka mafuta au losheni unayoitumia.

**MAZIWA MGANDO**

Maziwa mgando ni mazuri kwa kuondoa sugu kwenye miguu, chukua maziwa hayo paka kwenye miguu yako, acha kwa muda wa dakika 10-15 kabla ya kuosha.

Fanya hivyo kila unapokuwa na nafasi utaona jinsi utakavyo kuwa na ngozi laini isiyokuwa na sugu wala haina haja ya kwenda kuoshwa sehemu.

MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Kunywa juisi ya moto

JUISI ya chungwa yenye mchanganyiko wa asali ni kinywaji kizuri katika kipindi cha mapumziko hasa jioni.

Pia ni kinywaji mbadala unapoamka asubuhi badala ya chai,



maana hutumiwa ikiwa ya moto na hakuna sukari inayoongezwa.

**NAMNA YA KUANDAA**

Chukua machungwa yako kulingana na kiasi cha juisi unachotaka na asali kiwango unachopendelea.

Kamua machungwa yako na ukishapata juisi unayotaka usiongeze kitu kingine.

Unaweza kuandaa juisi hii kwa kuchanganya asali na kisha kuipasha moto.

Kama unatumia 'microwave' changanya juisi na asali na kisha weka kwa muda wa dakika moja hadi mbili ili ipate kuchanganyika vizuri.

Kama unatumia jiko la mkaa, changanya asali na juisi kisha weka kwenye sufuria na bandika jikoni kwa muda wa dakika tano hadi saba.

Acha ichemke vizuri ili asali na juisi zichanganyike vizuri. Unaweza kukoroga pia ili kusaidia mchanganyiko uwe sawia.

Asali ikiwa kwenye moto inapata kulainika, hivyo huchanganyika vizuri na juisi ya machungwa na kuipa utamu wa kipekee.

Kwa maana hiyo unaweza pia kutumia asali yenye mabonge maana italainika vizuri, kwani microwave pia hutumika kulainisha asali.

MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**



# Nyumba yako matokeo ya uchaguzi wako

## Jinsi ya kupangilia chumba cha mtoto wa kiume



Mapambo ya chumba cha watoto wa kiume ni jambo la kuzingatiwa na inaweza kukuza vyema akili zao. Kutokana na umuhimu wake hizi ni baadhi ya dondoo za namna ya kupamba chumba cha watoto wa kiume.

**1:** Paka rangi inayovutia chumbani, mara nyingi rangi ya bluu inapendwa na wengi kutokana na kuwa tulivu.

**2:** Weka wanasesere ambao wanaweza kumsaidia kukuza akili yake, unaweza kuweka magari, mipira na hata wanyama ili kumuongezea udadisi.

**3:** Weka kitanda kinachompa uhuru wa kupanda na kushuka, pamoja na kufanya mambo mengine kama kusoma au kula.

**4:** Usikifanye chumba kiwe kidogo, hakikisha kuna eneo pana la kumwezesha kucheza vizuri akiwa na wenzake.

NI ukweli usiopingika kuwa kila mtu anahitaji kuwa na nyumba bora, safi na salama kwa matumizi mbalimbali ikiwamo kuishi au biashara.

Mazingira safi na salama ni matokeo chanya ya kuwa na makazi bora na salama. Thamani ya maisha ya mtu ni nyumba.

Pia aina ya nyumba inayojengwa ni matokeo ya uchaguzi wa mhusika mwenyewe kutokana na matumzi yake.

Mtalaam wa ujenzi, Christopher Kimath, anasema kabla ya nyumba kujengwa ni umuhimu mhusika mwenye kutaka ajengewe nyumba awe na ndoto ya aina ya nyumba anayohitaji ili anapotafuta mtaalam wa kumjengea, ajue namna ya kuzungumza naye.

Anasema pamoja na mageuzi makubwa yaliyopo kwenye sekta hiyo ya ujenzi, bado kuna baadhi ya watu hawajafahamu namna bora ya kufanya uchaguzi kwa ajili nyumba za ndoto zao. Hata wanapokutana na wataalam wao wanashindwa kuwaeleza kwa usahihi aina ya nyumba wanazohitaji.

"Mtu amekutana na mtaalam kwa mara ya kwanza kwa ajili ya nyumba yake, lakini eti anapata kigugumizi cha kuzungumza. Badala ya kumweleza kwa usahihi nyumba anayotaka kujenga, anakuwa haeleweki. Wengine huwa wanakosa msimamo wa kufahamu hasa ni ya aina gani anayohitaji, kwa hiyo wakati mwingine kushindwa kueleweka na wataalam wao.

"Kwa hiyo inabidi mtaalam yeye ndiye atumie akili yake kuchagua na kuanza kuelekeza na kuna ambao hawaelewi kabisa mpaka nyumba ianze kujengwa ndio ataelewa, inakuwa ni mtihani mkubwa," anasema.

Kimath anasema miongoni mwa mambo unayopaswa kuzungumza na mtaalamu anayekujengea nyumba ni pamoja na mwonekano wa nyumba unayohitaji kwa kuwasilisha mapendekezo yako ya aina ambayo unaamini kuwa utaipenda na itakufaa kwa matumizi uliyokusudia.


"Vyovyote utakavyomweleza na kuuliza, yeye kwa sababu ni mtaalam na ana uwezo mkubwa wa kufanya chochote, inakuwa rahisi kufahamu namna ya kukusaidia na ikiwezekana kukuelimisha zaidi ili kufikia kile unachohitaji," anasisitiza.

Yapo mambo ambayo utayapenda lakini kwa wengine ni chukizo ndiyo maana ni vizuri kuzungumza na kusikilizwa kwa ajili ya kuboresha baadhi ya upungufu kama upo na kuboresha mwonekano wa nyumba.





# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2021
SMS - 0621 412 879
JUKWAANI
VIPI
'KIPI'
SIO SIRI MGONGO WOTE UNAPASUA! NAHISI KAMA NIME-BEBA KONTENA
SASA WENZETU HAYA MAKONTENA NDIO WANAYOISHI NAYO DEILE...
MKE WANGU NAJUA UNAJUA NIMEKAMATWA NA NYUMBA NDOGO, NAOMBA RADHI
UNAYAJUA MARUHANI YA KULE KWETU ' KANDA MAALUMU?'
TUMESHAELIMIKA MKIPOTEA NJIA HATUSUBIRI
TUNAMGANDA MAMA KWA KILA KITU KUMBE WEWE UPO UNAJENGA HESHIMA BAR!
NYIE MTAPATA TABU MAISHANI MWENU MIGUU NNAYO LAKINI MNANIGEUZA 'NYOKA'
NAKULAANI HADI MILELE... NIMEKUENDEKEZA MPAKA NAJIKUTA "HOHEHAHE!"
KILA SHETANI NA KITI WAKE "UTAKOMA"
KOMONI
NAONEKANA FISADI KUMBE APECHE ALOLO SINA LOLOTE!
UNAUHAKIKA SIO MURONGO? OPERESHENI HAIDANGANYWI UTAUMBUKA!
OPERESHENI
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...UNAPENDA MVUA UNAOGOPA KULOWA

HABARI KIMATAIFA

# Ujerumani wajadili serikali ya mseto

**BERLIN,** UJERUMANI

WAJUMBE wa Chama cha Kijani na wa Chama cha Waliberali (FDP), wameendelea na duru ya pili ya mazungumzo juu ya kuunda serikali ya mseto.

Majadiliano hayo yanafanyika baada ya kufanyika uchaguzi mkuu nchini Ujerumani.

Vyama hivyo vyenye karata za turufu katika mazungumzo hayo, vinajaribu kutafuta msingi wa pamoja na wajumbe wake wamesema wataweka mkazo katika sera kwenye mazungumzo.

Licha ya tofauti za kimsingi baina ya vyama vyao, mwenyekiti mwenza wa Chama cha Kijani, Robert Habeck, alisema wanatambua umuhimu wa mazungumzo hayo wanayofanya na kwamba ni muhimu kuleta mafanikio. Viongozi wa vyama vya Kijani na FDP wanatarajiwa kukutana pia na wajumbe wa vyama vya SPD na CDU wiki ijayo, katika juhudi za kuunda serikali ya mseto ambayo safari hii nchini Ujerumani itahitaji kuundwa na vyama vitatu.

# Rais Macron akasirishwa na serikali ya mpito ya Mali

**PARIS,** UFARANSA

RAIS wa Ufaransa, Emmanuel Macron, ameelezea kushtushwa kwake na kauli ya Waziri Mkuu wa Mali, Choguel Maïga, aliyoitoa kwenye kikao cha Umoja wa Mataifa na kuiita ni ya aibu.

Waziri Mkuu Maiga alielezea mpango wa Ufaransa kupunguza vikosi vyake katika eneo la Sahel vinavyoendelea na operesheni Barkhane, kukabiliana na wanamgambo wa kijihadi sawa na kuiacha Mali.

Rais wa Ufaransa alisema maneno ya kiongozi huyo wa mpito hayakubaliki.

"Nakumbusha kwamba Waziri Mkuu wa Mali ni mmoja walioshirikishwa katika majaribio mawili ya mapinduzi, ninaweza kusema hivyo. Kwa kuwa kulikuwa na mapinduzi Agosti, 2020 na ni mengine ndani ya mapinduzi. Kulingana na kanuni za kidemokrasia, serikali ya sasa si halali. Kauli yake hakikubaliki, ni aibu na inadhalilidha hata serikali. " alisema Macron.

Alisema kauli hiyo siyo raia wa Mali wanavyofikiria, kwa sababu wananchi ndio wahanga wa kwanza wa ugaidi wa kijihadi.

"Ninajua kuwa leo, wananchi wa Mali wengi wanafikiria watoto wao waliouawa na magaidi hawa, lakini pia wanafikiria familia hizi za wanajeshi ambao walipoteza ndugu zao kwa kutoka kwao kwenda umbali wa maelfu ya kilomita kusaidia kuokoa Mali. Kuna dharau nyingi kutoka kwa uongozi wa sasa wa Mali kwa wanajeshi wetu, haikubaliki. "aliongeza

Emmanuel Macron alisema hatarajii chochote kutoka kwa serikali ya Mali na kuongeza kuwa serikali hiyo ingepaswa kuheshimu ahadi zake ya kuandaa uchaguzi mwezi Februari na kuacha kuwaweka viongozi wa kisiasa gerezani.

# Merkel ataka mamluki Libya kuondoka haraka

**ERLIN,** UJERUMNI

WAKATI akijiandaa kuondoka madarakani, Kansela wa Ujerumani Angela Merkel, ametoa wito wa kuondolewa mamluki wote nchini Libya.

Akizungumza katika mkutano na Rais wa kipindi cha mpito nchini Libya, Mohammad Younes Mnefi, mbaye anafanya ziara nchini humo, Merkel, alisema mustakabali wa Libya unapaswa kujengwa na watu wa nchi hiyo bila ya ushawishi kutoka nje. Merkel pia alisisitiza umuhimu wa uchaguzi uliopangwa kufanyika Desemba 24, mwaka huu na ameahidi kuwa itaendelea kupewa kipaumbele. Ujerumani ni miongoni mwa nchi zinazosuluhisha katika mgogoro wa nchi hiyo ya Afrika kaskazini, baada ya kupinduliwa kiongozi wa muda mrefu Muammar Gaddafi mnamo mwaka 2011.

Libya iliingia kwenye vita vya wenyewe kwa wenyewe ambavyo vilijumuisha idadi kubwa ya wanamgambo na makubaliano ya kusimamisha mapigano yalifikiwa tangu mwaka jana na mapema mwaka huu serikali ya mpito iliundwa chini ya usimamizi wa Umoja wa Mataifa.

Mwaka jana, serikali ya Ujerumani ambayo imechukua jukumu la kuwa kama mpatanishi katika mzozo huo, iliandaa mkutano mkuu mjini Berlin lengo likiwa ni kumaliza hatua za nchi nyingine kuingilia kati mgogoro wa pamoja na uingizaji wa silaha na mamluki nchini humo.

Miongoni mwa nchi zilizohusika katika mgogoro wa Libya ni Urusi, Uturuki, Misri na Falme za Kiarabu.

Libya kwa miaka mingi imekuwa kitovu cha kuwasafirisha wahamiaji kutoka Afrika na Mashariki ya Kati wanaokimbia vita na umaskini katika nchi zao wakitumaini kuanza maisha bora barani Ulaya. Wafanyabiashara haramu wa kusafirisha watu wametumia machafuko ya nchini humo kujinufaisha kwa kuwasafirisha wahamiaji kwa kutumia boti za mpira au za mbao kupitia bahari ya Mediterrania.

Maelfu ya wahamiaji wamezama na kupoteza maisha huku wengine wakikamatwa na kurudishwa nchini Libya na kuwekwa mahabusu ambako mara nyingi watu hao huteswa na kulazimishwa kutoa fidia.

**DW**



Wakimbizi kutoka Haiti wakipambana na polisi wa Marekani katika mpaka wa nchi hiyo na Mexico wakati vurugu zilizotokea hivi karibuni katika kutekeleza mpango wa kuwarudisha nchini mwao **(PICHA: BBC)**

# Kanali Doumbouya aapishwa kuongoza Guinea

**CONAKRY,** GUINEA

KIONGOZI wa mapinduzi ya mwezi uliopita nchini Guinea, Kanali Mamady Doumbouya, amekula kiapo cha kuwa rais wa mpito.

Baada ya kukamilisha shughuli ya kuapa, Doumbouya aliahidi kuheshimu wajibu wa taifa hilo kimataifa, uaminifu na uhuru wa taifa hilo wakati wakielekea kukabidhi madaraka kwa serikali ya kiraia. Hata hivyo kwa mara nyingine hakuzungumzia kuhusu muda atakaoongoza kama kiongozi wa mpito.

Doumbouya aliyeongoza mapinduzi yaliyomuangusha Rais Alpha Conde, mnamo Septemba 5 mwaka huu, aliapishwa jana mbele ya kiongozi wa mahakama ya juu nchini humo, Mamadou Sylla. Hafla ya uapisho ilifanyika kwenye kasri la Mohammed-V, wakati nchi hiyo ikiadhimisha jana Uhuru wake kutoka utawala wa Ufaransa

**DW**

MAKALA

# MWOKA MIKATE MWENYE NJAA



Na Magabilo Masambu

HAPO zamani palikuwa na mtu mmoja aliyesifika sana katika kuoka mikate. Kilichowashangaza wateja wake na watu wengine katika kijiji kile ni kwamba mwoka mikate huyu kadri alivyokuwa akifanya kazi yake, ndivyo alivyoonekana kukonda zaidi. Baadhi ya watu walipofanya utafiti kwa nini alionekana hivyo, wakagundua kwamba anakonda kwa sababu ya njaa.

Maswali kadhaa yakajitokeza kwamba inawezekanaje mwoka mikate akonde kwa njaa ikiwa yeye ndiye mpika mikate? Ina maana anafanya kazi ya kuwauzia wengine mikate lakini yeye hali? Je, anakosa muda wa kula au anathamini fedha zaidi anazozipata kwa kuuza mikate au anawajali sana wateja wake?

Mwaka 1967 baada ya kutangazwa Azimio la Arusha, kuliibuka minong'ono na manung'uniko miongoni mwa viongozi wa chama na serikali juu ya miiko ya uongozi ndani ya Azimio la Arusha. Baada ya manung'uniko hayo kusikika, Mzee Rashidi Mfaume Kawawa, aliyekuwa Waziri Mkuu na Makamu wa Pili wa Rais, aliwatangazia wabunge kwamba kama wana maswali basi wayawasilishe na yatajibiwa na Rais Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.

Katika kuitikia wito huo, maswali 21 yaliwasilishwa ili yajibiwe na Mwalimu mwenyewe. Kwa mujibu wa Mwalimu ni kwamba maswali yote 21 yalihusu namna gani maisha ya viongozi yatakuwa baada ya uongozi wao. Hakuna lililohusu Ujamaa na Kujitegemea na hii ni kwa sababu ilionekana miiko kuwabana ili wasijitafutie maisha mengine nje ya uongozi kwa mujibu wa maelezo yao.

Kati ya maswali 21 yaliyowasilishwa, chafu kuliko mengine yote kwa maelezo ya Mwalimu ni lile lililosema; "Hali ya mwanasiasa haina uhakika, leo ni waziri kesho si waziri, leo ni mbunge baada ya miaka mitano si mbunge tena, leo ni katibu wa wilaya au mkoa kesho katupwa na wananchi kwenye uchaguzi. Je, azimio la Arusha haliwaonei viongozi hawa ikiwa litawazuia kujitengenezea maisha yao ya baadaye?"

Majibu ya Mwalimu katika swali hili yakawa haya: "Je, ni kiongozi gani miongoni mwenu ambaye wakati wa uchaguzi anawaambia wananchi wamchague ili ajitengenezee maisha yake ya baadaye? Ni nani ambaye alipata kazi katika TANU awe katibu wa wilaya au mkoa kwa lengo la kutengeneza maisha yake ya baadaye?

"Kila tunapotaka nafasi ya kisiasa japo ya kuchaguliwa kwa kura au kwa kuteuliwa husema tuchagueni tukuboreshea maisha yenu. Kiongozi ana haki gani basi mara tu baada ya kuipata nafasi hiyo kusema anataka kuitumia ili kutengeneza maisha yake ya baadaye?"

Nimeeleza hapo juu kuhusu habari ya mwoka mikate mwenye njaa. Si vyema na haki kumnyima mwenye njaa kuoka mikate japo hatutamruhusu ale mikate anayotengeneza kwa sababu anaweza kula mpaka akavimbiwa na mwisho wa siku asipate tena mikate ya kuuza ili apate fedha ya mahitaji mengine.

Lakini ni busara zaidi mwoka mikate kuwa ameshiba kwanza ili awe na nguvu zaidi ya kuoka mikate na mwisho wa siku asiweze kufanya kazi mpaka akafa njaa na wateja wakafa pia kwa kukosa mikate.

Katika nchi yetu, kwa miongo kadhaa, tumekuwa na dhana ya kuamini kwamba viongozi wazuri ni wale wanaotoka katika familia masikini. Hii ndiyo maana kila kiongozi anapotaka nafasi za kuchaguliwa, husikika akisema mimi ni masikini na kwamba maisha yenu nimeyaishi nipeni nafasi niwasaidie kwasababu shida nazijua. Ni kweli inawezekana shida unazijua ni jambo moja, lakini kutotumia nafasi yako ili kuondoa kwanza umasikini wako ni jambo la pili japo si wote wanafanya hivyo.

Upande wa pili tumekuwa na hofu na walioshiba, yaani wenye mali kwamba tukiwapa nafasi watatumia kujilimbikizia zaidi. Kosa kubwa tunalofanya ni kuwapima watu kwa umasikini au utajiri wa mali. Lakini masuala ya uongozi watu wanapaswa kuwa wameshiba zaidi katika eneo la uongozi, ziko wapi leo shule za uongozi? Au kinachotuongoza zaidi ni visomo vikubwa pekee visivyohusiana na uongozi? Yako wapi leo maadili na miiko ya uongozi?

Kwa hiyo kabla ya kuoka mikate, yafaa tuwe tumeshiba kwanza ili tupate nafasi bora ya kuwahudimia wateja wetu na kuepusha kutumia nafasi hizo kula mikate ya wateja na mwisho wa siku wateja watakufa kwa njaa au sisi wenyewe ikiwa tutaendelea kuifanya kazi bila kushiba kwanza.

Kinachoonekana sasa ni kwamba nafasi za uongozi ni mahali pekee pa kupata utajiri. Itatuchukua miaka mingi sana kuinua hali za watu wetu. Yako malalamiko huko mtaani, unakuta kuna mfadhili mahali fulani anataka kusaidia jambo fulani ama kutengeneza barabara au kuchimba kisima. Viongozi wenye njaa ndio wanakuwa wa kwanza kukwamisha mradi.

Wanakwamishaje? Eti mpaka mfadhili awape kwanza teni pasenti waweke mifukoni ndiyo jambo lifanyike! Tunawanyima maendeleo wananchi kwa sababu ya njaa zetu. Ni aibu sana. Eti mtu mmoja anaweza kuzuia maendeleo ya kijiji halafu ukifika wakati wa uchaguzi anakuja tena anasema mimi ni masikini nichagueni nazijua shida kumbe shida ni yeye.

Nafikiri kwenye kampeni muwe mnatuambia tu ukweli kwamba nichagueni maana watoto wangu wameshindwa kwenda shule, sijafanya hiki na kile ili tunapokuwa tunawapa nafasi basi tusiwadai baadaye maana tayari tunafahamu kwamba fedha zetu za maendeleo zina matumizi tayari.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**ARUSHA-TANZANIA**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Unajua Marijani, Meneti, Bitchuka walicheza soka?



Na Adam Fungamwango

HIVI karibuni klabu ya Simba ilipata pigo kufiwa na mmoja wa viongozi wake, aliyekuwa Mjumbe wa Bodi ya klabu hiyo, Zacharia Hans Poppe, aliyefariki usiku wa kumkia Septemba 10 kwenye Hospitali ya Aga Khan, Dar es Salaam, na kuzikwa mkoani Iringa.

Wengi wanamfahamu kama ni kiongozi, mwanachama na mpenzi wa klabu ya Simba na mmoja wa waanzilishi wa kundi la "Friends of Simba." Hao ni wengi zaidi kwa sababu umaarufu wake hasa kwa vijana wa sasa ulipatikana huko.

Kwa wale watu wa miaka ya nyuma, wanamfahamu Hans Poppe aliyekuwa mwanajeshi, aliyefikia ngazi ya Kapteni. Hawa wanamfahamu zaidi kwa kile kilichotajwa ni alikuwa mmoja wa watu waliotuhumiwa kuwemo kwenye jaribio la mapinduzi.

Sitaki kwenda huko sana. Nina upande fulani ambao wengi hawamfahamu Hans Poppe. Mbali na kuwa 'Mjeshi' na mpenzi wa mpira, alikuwa pia mwanamuziki.

Akisoma wasifu wa marehemu, mmoja wa viongozi wa klabu hiyo, Crescentius Magori, alisema wengi wanamfahamu Hans Poppe kwenye masuala ya soka, lakini kitu ambacho hawakifahamu ni kwamba alikuwa pia ni mwanamuziki mwenye uwezo mkubwa wa kupiga gita na alipigia bendi ya Safari Trippers.

Bendi hiyo ilivuma mno katikati ya miaka ya 1970 hadi mwisho, iliyokuwa ikiongozwa na David Mussa, mwimbaji mkuu akiwa ni marehemu Marijani Rajabu.

Kwenye mtandao wake wa kijamii, Msemaji wa Yanga, Haji Manara, wakati wa msiba wake, pamoja na kuandika wasifu wake kuwa ni mtu jasiri, mwenye msimamo, alimtaja kama ni mwana

"Usilolijua kuhusu yeye pia ni fundi wa kucharaza gita la solo na kwenye uvulana wake, akiwa bado mdogo alishiriki na bendi ya Safari Trippers kama mwanamuziki akiwa na Marijani Rajabu (naye sasa marehemu).

Tuachane na Hans Poppe sasa tuelekee kwa kwa mwanamuziki watatu maarufu nchini ambao nadhani kama wasingekuwa wanamuziki wangecheza soka kwa kiwango cha juu sana.

Hao ni Marijani, Hemed Maneti na Hassan Bitchuka. Leo sitaki kuwaeleza sana kuhusu kazi zao za muziki, ila yale ambayo wengi hawayafahamu.

Marijani, aliyezaliwa Machi 23, 1955 na kufariki dunia mwaka 1995. Aliondokea kuwa mwanamuziki mkubwa nchini ambaye hata watoto wanaokuwa leo wanakuja kukuta jina lake 'likiimbwa', pamoja na nyimbo zake kama 'Georgina', 'Siwema', 'Zuwena', 'Mwanameka' na 'Hanifa'.

Kifupi ni kwamba Marijani alikuwa mwanamuziki wa bendi za STC, Safari Trippers na Dar International. Alizaliwa Dar es Salaam maeneo ya Kariakoo. Alikuwa mtoto wa mjini haswa.

Wakati anaanza muziki, alikuwa pia golikipa mzuri mno. Alizidakia timu mbalimbali Karikaoo na Ilala, ikiwamo timu maarufu ya Kahe FC. Kuna wakati alikuwa akitoka kucheza mpira, anaoga na kwenda dansini. Alishaanza pia kudakia timu ya vijana wa Simba. Kutokana na mahaba yake na klabu ya hiyo, wengi walitarajia kuwa angekuja kuwa kipa wa Simba.

Hata hivyo, kwa kauli yake mwenyewe akiwa hai alisema sauti ya muziki iliizidi ya soka, hivyo akawa mwanamuziki.

Mwingine ni Hemed Maneti. Mwanamuziki mwimbaji wa bendi za Cuban Marimba, TP Limpopo za Morogoro na Vijana Jazz. Alifariki dunia Mei 31, 1990 kwenye Hospitali ya Mwananyamala, Dar es Salaam.

Mbali na kuimba na kutunga nyingi, Maneti aliyezaliwa Muheza Tanga, alikuwa pia mcheza soka mahiri. Huenda asingekuwa mwanamuziki, angekuwa mchezaji mzuri kama ambavyo angekuwa Marijani.

Historia inasema aliwahi kucheza timu moja ya Omari Gumbo ambaye baadaye alikuwa winga hatari wa Simba, lakini pia akaiongoza klabu hiyo ya Msimbazi. Waliachana Gumbo akaendelea na mpira, Maneti kwa kuwa alikuwa pia na kipaji cha muziki, akaendelea nacho. Haijajulikana Maneti alikuwa shabiki wa timu gani.

Mtoto wake aitwaye Maneti Hemed alichukua kipaji cha soka cha baba yake na kuchezea klabu mbalimbali, Dar es Salaam, ingawa hakubahatika kuchezea klabu kubwa.

Mwingine ni Bitchuka. Huyu kwa bahati nzuri yupo hadi leo. Pamoja na kuwa mwimbaji mwenye sauti nyororo, akizipigia bendi karibuni zote kubwa nchini, ikiwapo NUTA Jazz iliyokuwa ikimilikiwa na Jumuiya ya Wafanyakazi Tanzania na baadaye ikaitwa JUWATA kisha OTTU kwa sasa ni Jazz Msondo Ngoma Music Band. Pia alipigia Mlimani Park Orchestra, Orchestra Safari Sound na National Panasonic.

Historia yake inaonyesha kuwa alitoka Kigoma alikozaliwa kwenda Arusha kwa masuala ya soka, ingawa pia alikuwa anajua muziki, akitega kote kote.

Alikuwa winga hatari, hivyo alipata timu mjini Arusha, lakini wakati huo huo akiendelea na kipaji chake cha muziki, ndipo alipoonekana na kujiunga na bendi ya National ya huko. Ni bendi ambayo ilimfanya NUTA Jazz 'Msondo Ngoma' kumnyakua na safari ya ustaa ikaanzia hapo. Hadi leo ni mwanachama na shabiki wa klabu ya Simba.

**Kwa maoni piga 0716 350534**

# HADITHI

KWANI mapenzi ni nini? Si kumpenda yule unayemtaka wewe? Kwa nini inafika wakati watu wanapangiana? Je, ukilazimisha yanaitwa mapenzi? Si yatafanana na utumwa? Yeyote anayetaka kulifanya penzi liwe na matabaka, rangi, kabila, anaweza kusababisha maafa makubwa.

Donald. Kijana msomi aliyetoka nchini Marekani, anarejea nchini Tanzania. Akakabidhiwa kuendesha kampuni za baba yake. Lakini pia anatakiwa aoe. Hapo ndipo tatizo linapoanza. Usikose hata nakala moja ya riwaya hii tamu na ya kusisimua.

## Sumu ya mapenzi- 26

Mtunzi anapatikana (0716 350534)

**Na Adam Fungamwango**

HARAKA, Donald aliingia na kupenya kwa uangalifu mkubwa. Uzuri ni kwamba alikuwa akijua chumba kimoja baada ya kingine kwenye nyumba hiyo. Kabla ya kufika kwenye sehemu ya kulia chakula, alisikia maongezi. Kwa kawaida Doroth hukaa yeye, dada yake, na wafanyakazi wa ndani wawili, wa kike na wa kiume.

"Unasikia mpenzi, nia yangu ilikuwa ni kummaliza na kuchukua simu ili ushahidi ukosekane, lakini wale vijana niliowatumia kuna vitu walivikosea." Ilikuwa ni sauti nzito wa kiume.

"Chiko, wewe ndiyo umasababisha yote haya. Ni kweli Donald nilikuwa nampenda na nilitaka anioe, tukamuua yule dada kwa kushirikiana na baba yake mzazi, lakini sasa mambo yamekuwa magumu. Donald anajua kila kitu, hii ni hatari hasa kwangu, Ndiyo maana nimeona niachane naye, lakini auawe ili wewe sasa uwe na mimi, lakini hili naona nalo kama linashindikana." Alisikia sauti ya Doroth ikilalamika.

"Wewe unafikiri Donald ataongea chochote kwa polisi kwa sababu mmoja wa watuhumiwa ni baba yake?" Sauti ya mwanaume iliuliza.

"Na ndiyo kinaonekana kuchelewesha, lakini si umeona pale hospitalini, kuna polisi wanamlinda. Ni hivi Chiko, kama kweli unanitaka mimi, basi Donald afe, vinginevyo mimi nitakamatwa na utanikosa. Kweli nampenda Donald, lakini kwa hapa tulipofikia, kifo chake ndiyo usalama na amani kwangu."

"Basi mpenzi, yule nadhani ana siku mbili au tatu atoke hospitalini, atauawa tu, tena safari hii kwa mkono wangu."

"Jitahidi bwana."

Sasa hali haikuwa nzuri. Tayari Doroth anataka Donald auawe ili kuzima ushahidi wa kuonekana amehusika na mauaji wa Tausi. Lengo halikutimia. Awali hakutaka Tausi afe ili Donald arudishe mapenzi wake. Kilichotokea ni kwamba Donald akang'amua haraka kuwa yeye na baba yake mzazi ndiyo wamehusika kumuua mpenzi wake Tausi. Na sasa Doroth anaitafuta damu yake. Na kingine ni kwamba tayari ana mpenzi mwingine badala yake.

Hasira zilimpanda. Alichomoa bastola yake. "Mikono juu wote wawili." Aliamuru.




Doroth ambaye alikuwa akila chakula cha usiku na Chiko, mpenzi wake mpya.

Walionekana kushtuka. Hawakutegemea kupokea mgeni yeyote muda ule, hata wa heri, achilia mbali wa shari.

Waliacha kula. Wakainua mikono juu. Mmoja alikuwa ni mtu anayemjua vizuri Donald. Na mwingine alikuwa anamsikia tu.

"Nyie wauaji wakubwa. Doroth wewe ni mwanamke katili sana. Ndiyo maana nilisita kukupenda. Moyo wangu haukunituma kabisa kukuona wewe ni mwanamke wa maisha yangu. Kwa nini hukunipa uhuru, ukamchukua huyu kinyago wako na mimi kuniachia Tausi wangu? Ukamuua, halafu wewe leo uko na huyu mpumbavu mwenzako. Halafu akili zenu zilivyokuwa mbovu, unamtuma kuja kuniua mimi. Mkanitengenezea ajali ambayo nusu ichukue maisha yangu. Mna akili kweli nyinyi?"

Wakati Donald akifoka, huku akiwa amenyoosha bastoka yake kwa mkono wa kulia, ukiwaelekea Doroth na Chiko, hakutegemea kitu chochote ambacho kitaweza kumzuia kufanya analotaka kulifanya.

Ghafla, bila kutarajia akijikuta akipigwa na kitu ambacho hakukitarajia kwenye mkono ambao ulikuwa umeshika bastola. Kwa sababu hakutarajia, bastola ikamponyoka na kuanguka chini.

Ilikuwa kama ndoto. Sekunde chache baadaye ni yeye ndiye aliyekuwa amewekwa chini ya ulinzi.

Hakutarajia mbinu na ustadi wa hali ya juu uliofanywa na Chiko. Kwa akili ya haraka haraka alijua kabisa kuwa Donald angeweza kulipiza kisasi kwa kuwafyatulia bastola na kuwaulia mbali.

Hakuwa mtu wa mchezo mchezo. Kilikuwa ni kitendo bila kuchelewa, Chiko alijaribu bahati yake ya kukiepuka kifo, kwa kunyakua ghafla bakuli la kioo lililokuwa na mboga, na kmrushia Donald. Shabaha kwake kilikuwa kitu cha kawaida, kwani alikuwa na uwezo mkubwa wa kutumia silaha.

Ni bakuli zito la kioo lililokuwa kimejaa nyama na chuzi, ndilo lilipompiga mikono Donald na kuangusha bastola yake. Hapo hapo, Chiko ndipo alipotoa bastola yake na kumuweka Donald chini ya ulinzi.

"Sasa wewe ndiyo umejileta kwenyewe kwenye mdomo wa kifo." Chiko aliunguruma. "Piga magoti." Alimuru na Donald akatii. "Chukua ile bastola pale." Alitumwa Doroth na akatekeleza.

"Ndugu yangu una bahati mbaya sasa. Umejileta mwenyewe kwa mtu katili duniani kuliko ambao umepata kuwaona."

"Doroth kwani huyu ni nani?" Aliuliza akiwa amepiga magoti na mikono ikiwa juu.

"Unauliza jibu. Huyu ni bwana a'ngu, ndiye ambaye anataka kunioa."

"Ina maana mimi ulikuwa unanidanganya eee." "Wewe baba wee. Wewe mwenyewe muda si mrefu umesema moyo wako haukuwa unanipenda. Nikwambie tu ukweli. Mimi nilikuwa nakupenda sana Don. Upendweje mwanaume wee, nimefanya kila njia nimeshindwa. Nikaamua nimuue yule demu wako..."

"Kumbe ni kweli umemuua?"

Doroth alicheka kicheko cha dharau. "Usinichekeshe, unataka kusema we hujui. Unajua hasa, na tumeshirikiana na baba 'ako. Wazazi wako walinitaka mimi niwe mkeo, lakini wewe hukutaka. Tulijua tukimuua penzi litarudi kwangu, lakini wapi, hupendeki. Tena kibaya sasa tukagundua kuwa umeshafahamu kuwa sisi ndiyo wauaji. Baba yako alikuacha, lakini mimi nikatafuta njia ya kutaka nikunyamazishe kwa sababu ulionekana bado huko tayari kuwa na mimi."

> **"Chiko, wewe ndiyo umasababisha yote haya. Ni kweli Donald nilikuwa nampenda na nilitaka anioe, tukamuua yule dada kwa kushirikiana na baba yake mzazi, lakini sasa mambo yamekuwa magumu.**

"Kwa hiyo njia yenyewe ndiyo hii?"

"Ndiyo. We ulitakaje. Nimempata mchumba, anataka kunioa, lakini nimemwambia ili tuishi kwa amani ni lazima uawe nikamuelezea kila kitu, sikumficha."

"Ndiyo akanitengenezea ajali siyo?"

"We ulitakaje. Ndiyo. Tulitaka ufe na pia niligundua kuwa ulizipata meseji zetu tulizokuwa tunatumiana na baba yako, kwa hiyo ile ajali ilikuwa ya kuua na kuipata simu yako, ili tuichukue zisiende sehemu ambayo si nzuri kwa usalama wangu."

"Hivi unadhani ukiniua mimi ndiyo siri hii haitafichuka?"

"Nani atajua?"

"Baba si atajua umeniua na yeye anajua kila kitu?"

"Tumeua naye, halafu kwa taarifa yako tukikumaliza, tunakwenda kumaliza wazazi wako. Unadhani baada ya hapo nani atajua tena. Kinachofuata hapo ni ndoa tu.

Mshtuko ulimpata Donald. Pamoja na kufahamu kuwa Doroth ametekeleza mauaji ya Tausi, lakini hakutegemea kuwa angekuwa katili kiasi hiki.

Kumbe baada ya Tausi, sasa ameamua kumuua yeye na wazazi wake. Hilo lilimtisha zaidi kuliko kifo chake kitakavyokuwa.

"Sikiliza wewe." Sasa ilikuwa sauti ya Chiko. Nitakutandika bastola ya kichwa. Utakufa, halafu tutakwenda kukutupa baharini uwe chakula cha samaki. Sidhani kama polisi au mtu yeyote atajua nini kimetokea. Mimi ndiyo pia nitawaua wazazi wako. Nitajua watakufa kwenye mazingira gani, lakini lazime wawe marehemu." Aliongea kwa kujiamini.

"Simu yangu mliipata?" Aliuliza.

"Tuuulize wewe?"

"Sikuiona."

"Na ndicho tulichokuwa tunakitaka. Nilituma vijana waitafute na walikusachi sana ulipokuwa umepata ajali hawakuiona. Tukajua tu itakuwa imesagikasagika. Ila walikuwa waoga, walidhani umeshakufa, wangekuulia pale pale." Chiko alijigamba.

"Doroth nakuomba, niueni mimi, lakini msiniulie wazazi wangu."

Vicheko kutoka kwa wapenzi wawili Doroth na Chiko vilitawala.

"Utakuwa umeshakufa. Huna haki ya kutaka kujua tena duniani kuna nini. Ukishakufa, huku duniani tuachie wenyewe tujue nini tutafanya." Chiko aliongea kwa kejeli.

ITAENDELEA JUMAPILI



# JBWAI, STAA WA CAMEROON ANAYEMUOTA DIAMOND

BARA la Afrika halijawahi kukauka vijana wenye vipaji ambao wanafanya sanaa zao ndani na nje kwa mafanikio makubwa.

Miongoni wa vijana hao ni Jbwai, msanii wa kizazi kipya kutoka Cameroon ambaye kwa sasa anafanyia shughuli zake nchini Canada.

Yafuatayo ni maswali na majibu kama alivyofanya mahojiano maalum na NIPASHE hivi karibuni.

SWALI: Kwa ufupi Jbwai ni nani na uliingia vipi kwenye sanaa?

Jbwai: Mimi ni mwanamuziki wa Cameroon, mwimbaji, mtunzi wa nyimbo, mtayarishaji wa muziki niliyezaliwa Septemba 28, 1993. Nilianza kazi yangu ya muziki nilipohamia Toronto Canada, ingawa historia yangu ya muziki ilianza nikiwa mdogo.

**SWALI:** Je unakabiliwa na changamoto gani katika muziki wako ndani na nje ya Canada?

**Jbwai:** Changamoto yangu kubwa kama msanii wa kiafrika aliyeko Canada ni kwamba sijaunganishwa moja kwa moja na wale mashabiki ambao ni watu wa Afrika wanaoweza kuhusika kwa urahisi kuupaisha muziki wangu.

**SWALI:** Je! Ungependa kufanya kazi na wanamuziki gani kutoka Tanzania na Afrika Mashariki?

**Jbwai:** Msanii wangu anayependwa zaidi nchini Tanzania ambaye napenda kufanya muziki naye ni Diamond Platnumz, ingawa kuna wasanii wengine kama Harmonize na Rayvanny nina mipango ya kufanya nao kazi hapo mbeleni.

**SWALI:** Hadi sasa mafanikio gani umepata kupitia muziki wako?

**Jbwai:** Katika kazi yangu ya muziki, nimekuwa na mafanikio mazuri. Nimekuwa na maonyesho mazuri pia nimejenga uhusiano mzuri na watu wengu ambao wamenipa faida kubwa.

**SWALI:** Kwa nini ulifikiria kukuza muziki wa Afrika?

**Jbwai:** Afrika ndio mahali ambapo watu wanaupenda zaidi muziki wangu.

**SWALI:** Una mipango gani kwa mwaka huu kutembelea nchini Tanzania?

**Jbwai:** Katika miezi ijayo mpango wangu ni kutembelea Tanzania, kuwa na maonyesho kadhaa na kujiunganisha na mashabiki wangu na kujifunza utamaduni wa huko ambao naamini nitaufurahia.

# Fahyma kweli mapenzi yana wenyewe

MAMA mtoto wa Rayvanny, anayejulikana kama Fahyma, ameibuka na kumpamba mpenzi wake huyo wa zamani kwamba ni mwanaume aliyekamilika.

Fahma amesema kupitia akaunti yake ya Instagram, akisema mwanamuziki huyo ni kiboko wa Paula na kuwa upande wake lazima ampe sifa.

"Bado naendelea kumsifia, mwanaume aliyekamilika kwa upande wangu sijui kwa wengine, ila kwangu bado ni mtu muhimu sana, sababu roho ya mtoto wangu ni yangu pia", ameandika.



# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### STERLING HAKIELEWEKI

WINGA wa England, Raheem Sterling mwenye umri wa miaka 26, bado anakabiliwa na sintofahamu kuhusu siku zake zijazo pale Manchester City licha ya "mkataba usio rahisi " na kocha wa klabu hiyo, Pep Guardiola. ***(Daily Telegraph)***

### VLAHOVIC AITAMANI CITY

MSHAMBULIAJI wa Fiorentina na Serbia, Dusan Vlahovic mwenye umri wa miaka 21, ana ndoto za za kuhamia Manchester City. Mabingwa hao wa Ligi Kuu ya England walihusishwa na uhamisho wa mchezaji huyo kipindi cha msimu uliopita. ***(Gazzetta dello Sport)***

### HENRY AMKOSOA WENGER

THIERRY Henry amekosoa mpango wa kocha wa zamani wa Arsenal, Arsene Wenger wa kutaka michuano ya Kombe la Dunia ifanyike kila baada ya miaka miwili na kusema "unachosha akili". ***(Sun)***

### SOLSKJAER AMVAA SANCHO

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer amemwambia winga wa England mwenye umri wa miaka 21, Jadon Sanch kuwa mkweli, wakati akisubiri bao lake la kwanza katika klabu hiyo. ***(Mirror)***

### WERNER HALI TETE

MSHAMBULIAJI wa Chelsea na Ujerumani, Timo Werner, mwenye umri wa miaka 25, anakabiliana na kupambania hali yake ya baadaye katika klabu hiyo baada ya kuhangaika kuimarika tangu kuwasili kwa Romelu Lukaku. ***(London Evening Standard)***

### TORRES ANUKIA CITY

KLABU ya Manchester City inaangalia uwezekano wa kumsajili nyota wa Villarreal na Hispania, Pau Torres, mwenye umri wa miaka 24. ***(Marca)***

### MOURINHO AMTAKA NDOMBELE

JOSE Mourinho anapanga mpango wa kushitukiza wa kukutana tena na mshambuliaji wa Tottenham, Tanguy Ndombele mwenye umri wa miaka 24 ili atue kule AS Roma. ***(Calciomercarto via Express)***

### EVERTON YAMWANIA LONGSTAFF

HUENDA Everton wakamnunua kiungo wa kati wa Newcastle, Sean Longstaff mwenye umri wa miaka 23. ***(Independent)***

### MADRID WAKOMAA NA HAALAND

REAL Madrid watakuwa na fedha za kumnunua mshambuliaji wa Borussia Dortmund, Erling Haaland, mwenye umri wa maika 21 msimu ujao, huku wakiendelea kuwa na nia ya kumsajili nyota wa Paris St-Germain na Ufaransa, France star Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 22. ***(AS)***

### TUANZEBE ATAKA KUBAKI VILLA

MLINZI wa England, Axel Tuanzebe mwenye umri wa miaka 23, yuko wazi kuufanya mkataba wake wa mkopo pale Aston Villa akitokea Manchester United kuwa wa kudumu. ***(Birmingham Mail)***

## DONDO A SOKA
## MAGA AYA



# GUARDIOLA: KLOPP AMENIFANYA BORA

### Amebainisha hayo wakati Liverpool leo itakuwa nyumbani kuikaribisha Man City...

**LIVERPOOL,** England

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, amesema upinzani wake na Jurgen Klopp wa Liverpool umemfanya yeye kuwa "kocha bora."

**City imepitwa pointi moja na vinara wa Ligi Kuu England, Liverpool na timu hizo zinakutana leo Jumapili pale kwenye dimba la Anfield katika mchezo wa Ligi Kuu ya England, EPL.**

Wakati ambao City ilikosa ubingwa wa Ligi Kuu kwa kipindi cha miaka mine iliyopita ni pale Wekundu hao walipoutwaa msimu wa 2019-20.

"Tangu nimewasili hapa - pengine sio mwaka wa kwanza - mara zote Liverpool walikuwa na nafasi kubwa," amesema Guardiola akinukuliwa na BBC Sport.

Raia huyo wa Hispania, ambaye alichukua mikoba ya kuinoa City kipindi cha majira ya joto mwaka 2016, pia alikabiliana na Klopp, ambaye alikuwa kocha wa Liverpool Oktoba 2015, wakati akiwa kocha wa Bayern Munich na Mjerumani huyo akiinoa Borussia Dortmund.

Guardiola amepoteza mechi nane kwenye mashindano yote dhidi ya Klopp, ikiwa ni mara nyingi zaidi kuliko kocha mwingine yoyote.

"Timu ya Jurgen Klopp imenisaidia mimi kuwa kocha bora," alisema Guardiola, ambaye kikosi chake kitaingia kwenye mchezo huo dhidi ya Liverpool baada ya kuifunga Chelsea kwenye Ligi na kupoteza kwenye Ligi ya mabingwa Ulaya wakati walipofungwa na Paris St-Germain katikati ya wiki.

"Ameniweka mimi kwenye daraja jingine kabisa, nafikiri amenisaidia zaidi kuimarika kama kocha na kuwa bora. Hii ndio sababu kwanini hadi sasa bado nipo kwenye kazi hii.

"Miaka minne iliyopita, wote na muda wote tulikuwa hapa. Ni jambo zuri kwamba klabu zote mbili zilikuwa kwenye nafasi kubwa.

"Lakini kwenye Ligi Kuu England hakuna timu moja au mbili tu, kuna timu nyingi ambazo zinaweza kupambania ubingwa wa Ligi."

Liverpool ilifungwa mabao 4-1 pale kwenye dimba la Anfield kwenye mchezo wa Ligi, Februari wakati timu hizo zilipokutana na Klopp anajua kwamba, timu yake inatakiwa kuwa kwenye kiwango chake wakati ikiivaa City.

"Kwa hakika huu ni mchezo maalumu kila mwaka. Unatakiwa kuwa kwenye ubora wako," alisema Klopp akinukuliwa na BBc Sport.

CHEZA USHINDE KASINO

MECHI KALI
HOME AWAY
LIVERPOOL
2.79 | 3.39 | 2.49
MANCHESTER CITY

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa, vodacom m-pesa, halopesa, airtel money, ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# KAGERE AJIWEKEA UFALME



**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA wa Simba, Meddie Kagere, ameweka rekodi ya kuwa mfungaji wa bao la kwanza kwenye kikosi cha Simba kwa misimu mitatu, tangu alipojiunga na kikosi hicho akitokea Gor Mahia ya Kenya mwaka 2018.

Juzi Ijumaa, kwenye Uwanja wa Jamhuri Dodoma alipachika bao pekee dakika ya 70, Simba ikiichapa Dodoma Jiji 1-0 kwenye mechi ya raundi ya pili ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyoanza mwanzoni mwa wiki hii.

Lilikuwa ni bao la kwanza kwa timu hiyo, kwani kwenye mechi ya ufunguzi Simba ilitoka suluhu na Biashara United.

Hii ni mara ya tatu kwa misimu minne kwa Kagere kufanya hivyo, kwani msimu wa 2018/19 alikuwa pia mchezaji wa kwanza wa Simba kufunga bao la msimu huo kwenye dakika ya pili ya mchezo, Simba ikicheza dhidi ya Prisons, Uwanja wa Benjamin Mkapa na kuwa bao pekee. Mechi hiyo ya ufunguzi, ilichezwa Agosti 22, 2018.

Msimu uliofuata, Kagere tena alikuwa mchezaji wa kwanza kufunga bao kwa Simba, kwenye dakika ya kwanza, ikiwa ni mechi ya kufungulia msimu huo Agosti 29, msimu wa 2019/20, aliifanya timu yake kuondoka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya JKT Tanzania.



# Baraza awapa somo Biashara kimataifa

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Kagera Sugar, Francis Baraza, ameiangalia timu yake ya zamani ya Biashara United na amedai kwamba, wanakazi kubwa hasa katika safu ya ulinzi katika michuano ya kombe la Shirikisho Barani Afrika.

Akizungumza na gazeti hili jana, Baraza alisema anaipa nafasi kubwa Biashara kufanya vizuri katika michuano hiyo endapo safu ya ulinzi watakuwa makini na tulivu.

Alisema amepata bahati kuangalia kikosi cha timu hiyo vizuri tangu walipocheza mechi ya kwanza dhidi ya FC Dikhil ya Djibout na kuona upungufu wa Biashara United katika safu ya ulinzi.

“Hatua wanayocheza sasa sio rahisi ukiangalia soka limekuwa kubwa sana, Libya wako vizuri katika mpira hivyo Biashara United wanatakiwa kuwa makini hasa safu ya ulinzi,” alisema Baraza aliyewahi kukinoa kikosi cha Biashara msimu uliopita.

## HABARI MICHEZO

LIVE IN PLAY

# TREZEGUET: LUKAKU ANAHITAJI SAPOTI



**LONDON,** England

ROMELU Lukaku anahitaji sapoti kutoka kwa wachezaji wenzake pale Chelsea, kwa mujibu wa mchezaji wa zamani wa timu ya taifa ya Ufaransa, David Trezeguet.

Lukaku alirudi Stamford Bridge Agosti mwaka huu kwa ada iliyoweka rekodi klabuni hapo ya pauni milioni 97.5 akitokea Inter, akiwa amefunga mabao 24 katika mechi 36 za Serie A kipindi Nerazzurri hao wakishinda taji la Ligi Kuu msimu wa 2020-21.

Fowadi huyo wa Ubelgiji amefunga mabao manne katika mechi nane kwenye mashindano yote kwa Blues hao, likiwemo la ushindi dhidi ya Zenit kwenye mchezo wa ufunguzi wa Ligi ya mabingwa Ulaya hatua ya makundi.

Bao lake la kichwa dhidi ya klabu hiyo kutoka nchini Urusi lilimfanya kuwa mchezaji wa pili kuifungia klabu ya England kwenye mechi ya ufunguzi ya mashindano hayo, lakini Lukaku alishindwa kufanya hivyo wakati wakifungwa 1-0 na Juventus, Jumatano.

Nyota wa zamani wa Juventus, Trezeguet anaamini Lukaku anahitaji msaada zaidi kutoka kwa wachezaji wenzake wa Chelsea kama kikosi hicho cha kocha, Thomas Tuchel kinataka kupata ubora wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28.



# Iniesta aitamani Barca

**BARCELONA,** Hispania

GWIJI wa Barcelona, Andres Iniesta amesema "natamani" siku moja kurudi Camp Nou baada ya kutundika daruga.

Kiungo huyo wa kati alicheza mechi 674 akiwa na jezi ya Blaugrana hao kwenye mashindano yote kwa kipindi cha miaka 16 akicheza timu ya wakubwa, akifunga mabao 57.

Katika umri wa miaka 37, raia huyo wa Hispania bado anaichezea timu ya Vissel Kobe ya nchini Japan, akiwa amejiunga nayo kutoka Barcelona mwaka 2018, na ameshinda taji la Mfalme na la Super tangu ajiunge na kikosi hicho.

Mkataba wake na klabu hiyo ya Ligi Kuu ya Japan unamalizika Januari 2024, ambapo pengine mkongwe huyo anaweza kustaafu na kurudi kule Katalunya.

"Ndio, (kurudi Barcelona) ni kitu ninachokipenda," alisema Iniesta akiiambia BBC.

"Ningependa itokee hiyo siku moja kwa sababu ni klabu ambayo nilitumia muda na miaka mingi pale.

"Huwezi kujua nini kitatokea kwa siku za usoni, huwezi kujua utarudi kwa njia gani au nani atakuwa kocha wakati huo.

SPORTPESA APP
BET LEO UWE MILIONEA

PAKUA SASA

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMAPILI - 03 - OKTOBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:30 | 2782 | Bologna vs Lazio | 3.25 | 3.65 | 2.11 |
| 14:00 | 3329 | Rennes vs Paris St Germain | 4.90 | 4.14 | 1.61 |
| 15:00 | 5923 | Elche vs Celta Vigo | 3.36 | 3.11 | 2.29 |
| 15:30 | 2977 | Ajax vs Utrecht | 1.15 | 7.69 | 12.82 |
| 15:30 | 3712 | Cambuur vs AZ Alkmaar | 3.84 | 3.84 | 1.80 |
| 16:00 | 1046 | Lorient vs Clermont Foot | 2.38 | 3.35 | 2.90 |
| 16:00 | 1102 | West Ham vs Brentford | 1.80 | 3.66 | 4.41 |
| 16:00 | 3043 | Crystal Palace vs Leicester | 3.07 | 3.32 | 2.34 |
| 16:00 | 3614 | Monaco vs Bordeaux | 1.40 | 4.76 | 7.14 |
| 16:00 | 3779 | Verona vs Spezia | 1.66 | 4.13 | 4.73 |
| 16:00 | 4022 | Fenerbahce vs Kasimpasa | 1.48 | 4.34 | 5.92 |
| 16:00 | 4507 | Tottenham vs Aston Villa | 2.12 | 3.46 | 3.41 |
| 16:00 | 4995 | Sampdoria vs Udinese | 2.16 | 3.30 | 3.45 |
| 16:00 | 5552 | Nantes vs Troyes | 1.77 | 3.54 | 4.58 |
| 16:00 | 5611 | Angers vs Metz | 1.96 | 3.29 | 3.99 |
| 16:30 | 3220 | Mainz vs Union Berlin | 2.06 | 3.28 | 3.63 |
| 16:30 | 5317 | Zenit St Petersburg vs Sochi | 1.39 | 4.81 | 6.88 |
| 17:00 | 3420 | Rangers vs Hibernian | 1.36 | 4.83 | 7.50 |
| 17:00 | 5450 | Midtjylland vs Aarhus | 1.72 | 3.65 | 4.53 |
| 17:15 | 3464 | Espanyol vs Real Madrid | 4.70 | 3.84 | 1.72 |
| 17:30 | 3314 | Servette Geneva vs BSC Young Boys | 3.95 | 3.80 | 1.79 |
| 17:30 | 5299 | FC Basel vs FC Luzern | 1.44 | 4.86 | 5.75 |
| 17:45 | 4968 | Vitesse Arnhem vs Feyenoord | 3.25 | 3.84 | 1.97 |
| 18:00 | 2043 | Lille vs Marseille | 2.41 | 3.23 | 2.93 |
| 18:00 | 2969 | RB Salzburg vs LASK Linz | 1.26 | 5.62 | 8.14 |
| 18:15 | 4398 | OFI Crete vs PAOK | 5.31 | 3.34 | 1.70 |
| 18:30 | 2458 | Liverpool vs Manchester City | 2.79 | 3.39 | 2.49 |
| 18:30 | 3484 | Malmo vs Mjallby | 1.32 | 4.84 | 7.75 |
| 18:30 | 5794 | Bayern Munchen vs Eintracht Frankfurt | 1.14 | 8.76 | 12.94 |
| 19:00 | 1734 | Fiorentina vs Napoli | 3.86 | 3.61 | 1.93 |
| 19:00 | 3153 | Stabaek vs Bodo Glimt | 5.51 | 4.63 | 1.48 |
| 19:00 | 3234 | Randers vs Brondby | 2.28 | 3.41 | 2.91 |
| 19:00 | 3926 | Caykur Rizespor vs Galatasaray | 4.62 | 3.74 | 1.69 |
| 19:00 | 5112 | Odd Ballklubb vs Molde | 3.84 | 4.04 | 1.76 |
| 19:00 | 5895 | Roma vs Empoli | 1.41 | 5.21 | 6.42 |
| 19:30 | 3583 | Getafe vs Real Sociedad | 3.61 | 3.11 | 2.19 |
| 19:30 | 5520 | Villarreal vs Betis | 1.95 | 3.67 | 3.72 |
| 19:30 | 5629 | Royal Antwerp vs KAA Gent | 2.61 | 3.70 | 2.37 |
| 20:00 | 4954 | Sparta Prague vs Slavia Prague | 2.91 | 3.51 | 2.32 |
| 20:00 | 5635 | Benfica vs Portimonense | 1.20 | 6.10 | 12.79 |
| 20:30 | 4738 | Olympiakos vs Panathinaikos | 1.44 | 4.15 | 7.11 |
| 20:30 | 5292 | Arminia Bielefeld vs Bayer Leverkusen | 4.78 | 3.93 | 1.66 |
| 21:00 | 1038 | Copenhagen vs Viborg FF | 1.54 | 4.34 | 5.13 |
| 21:00 | 1347 | PSV Eindhoven vs Sparta Rotterdam | 1.19 | 6.52 | 11.85 |
| 21:00 | 1385 | Kristiansund vs Rosenborg | 2.56 | 3.50 | 2.51 |
| 21:45 | 2084 | St Etienne vs Lyon | 4.09 | 3.89 | 1.78 |
| 21:45 | 4559 | Atalanta vs AC Milan | 2.11 | 3.62 | 3.27 |
| 22:00 | 2951 | Eupen vs Racing Genk | 3.16 | 3.80 | 2.02 |
| 22:00 | 5249 | Granada vs Sevilla FC | 4.82 | 3.51 | 1.78 |
| 22:30 | 4462 | Sporting Braga vs Boavista | 1.48 | 4.34 | 5.92 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Jumapili Oktoba 3, 2021
Nipashe



Fahyma kweli mapenzi yana wenyewe UKURASA 20



Mshambuliaji wa Manchester United, Ednson Cavani, akiwania mpira dhidi ya beki wa Everton wakati wa mchezo wa Ligi Kuu England baina ya timu hizo jana Jumamosi, kwenye uwanja wa Old Trafford mjini Manchester. Timu hizo zilitoka sare ya kufungana bao 1-1. **PICHA: MTANDANO**

## Stars yaingia kambini kuiwinda Benin

**Na Saada Akida**

KIKOSI cha timu ya Taifa ya Tanzania, 'Taifa Stars' kinaingia kambini leo na kesho wataanza mazoezi kwa ajili ya maandalizi ya mchezo dhidi ya Benin utakaopigwa Oktoba 7, mwaka huu katika dimba la Benjamin Mkapa.

Mchezo huo ni wa kutafuta tiketi ya kufuzu michuano ya kombe la dunia itakayofanyika mwaka 2022 nchini Qatar.

Stars inaongoza katika msimamo wa kundi lake la J ikiwa na pointi nne sawa na Benin inayoshika nafasi ya pili, mchezo wa marudiano utapigwa Oktoba 10, Mwaka huu.

Timu ya Taifa ya DR Congo ina pointi mbili ikiwa nafasi ya tatu, huku Madagascar wakishika mkia katika kundi hilo kwa kutokuwa na pointi baada ya michezo yake miwili.

Kocha wa Taifa Stars, Kim Poulsen amesema timu hiyo itaingia kambini leo na kesho Jumatatu watafanya mazoezi ya kujiandaa na mchezo wao huo dhidi ya Benin.

Alisema wanahitaji kuwa makini kwa mchezo dhidi ya Benin, kwa sababu ni timu nzuri na asilimia 90 ya wachezaji wa timu hiyo wanacheza soka la kulipwa Ulaya, tofauti na Stars ambayo asilimia 90 wanacheza soka nyumbani.

"Hii ni mechi ngumu kutokana na wapinzani wetu, lakini tunajipanga kuhakikisha tunapambana kwenda kutafuta ushindi katika kila mechi ili kutafuta tiketi ya kufuzu kucheza kombe la Dunia," alisema Poulsen.

Wachezaji walioitwa Stars ni Aishi Manula (Simba), Metacha Mnata (Polisi Tanzania), Ramadhan Kabwili (Yanga), Shomari Kapombe, Erasto Nyoni (Simba), Dickson Job na Bakari Nwamnyeto (Yanga), Kenedy Juma (Simba), Lusajo Mwaikenda (Azam FC), Mohammed Hussein'Tshabalala' (Simba).

Edward Manyama (Azam FC), Nickson Kibabaje (KMC) Meshack Mwamita (Gwambina FC), Novatus Dismas (Maccabi Tel Aviv-Israel), Mzamiru Yassin na Jonas Mkude (Simba).

Wengine ni Feisal Salum (Yanga) John Bocco (Simba) Iddy Seleman Musa na Abdul Hamis Seleman (Azam FC), Mbwana Samatta (Royal Antwerp-Ubelgiji), Reliants Lusajo (Namungo FC) na Simon Msuva (Wydad AC-Morocco).

# Gomes: Ligi sasa imekuwa vita

**Na Saada Akida**

### Alia na faulo za wachezaji wa Dodoma, asema Simba imejipanga kupambana, ajivunia kikosi chake...

KOCHA Mkuu wa Simba, Didier Gomes, amesema Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu itakuwa kama vita na kikosi chake kipo tayari kwa ajili ya kupambana.

**Akizungumza na gazeti hili jijini jana baada ya kikosi cha Simba kurejea jijini Dar es Salaam wakitokea Dodoma, Gomes alisema wanacheza mechi ngumu sana na wako tayari kupambana na aina ya ligi ya msimu huu kwa wapinzani wao wakicheza kwa kukamia.**

Alisema mechi dhidi ya Dodoma jiji FC, timu yake ilionesha kiwango kizuri, lakini amesikitishwa na wapinzani wao kuwafanyia faulo za wazi nyota wake na baadhi kushindwa kuendelea na mchezo.

"Tumejua aina ya ligi ambayo tutacheza msimu huu, hii ligi itakuwa ni kama vita, lakini nina uhakika Simba imejipanga, tunacheza mechi ngumu sana tuko tayari kupambana na hilo ndio naweza kusema, najivunia sana wachezaji wangu," alisema Gomes.

Alisema kilichoonyeshwa na wachezaji wake katika michezo miwili waliocheza dhidi ya Biashara United na Dodoma, ndio mwanzo wa msimu baada ya kupitia changamoto kubwa katika wiki iliyopita.

"Nimefurahishwa na wachezaji wangu walivyopambana kupata matokeo yamerudisha morali yetu baada ya kutoka katika kipindi kigumu, tupo kwenye wakati mgumu tuna wachezaji wengi majeruhi wengi wao wamepatikana katika mchezo huu dhidi ya Dodoma jiji, sijui kama ilikuwa lengo la wapinzani wetu kufanya hivyo," alisema Gomes.

Alisema Kennedy Juma, Pape Sakho na Taddeo Lwanga walifanyiwa faulo na kushindwa kuendelea na mchezo huo, lakini kwa sasa wanaendelea vizuri baada ya kupelekwa hospital baada ya kuumia katika mchezo huo.

Kocha huyo alisema baada ya vipimo vya daktari nyota wao wawili, Kennedy na Sakho wanaendelea vizuri na wamepewa mapumziko ya siku chache wakiwa chini ya uangalizi wa daktari kabla ya kurejea mazoezi huku Taddeo yuko fiti.

Simba imerejea na ushindi wa bao 1-0, lililofungwa na Meddie Kagera, ushindi wa kwanza kwa timu hiyo baada ya kupata suluhu tasa dhidi ya Biashara United mchezo uliofanyika katika uwanja wa Karume.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >